# Nipashe

Jumatano Mei 5, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580571

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





**Bunge** lataka taarifa fedha za miradi ya maji kutoka Misri

UKURASA 3



**BAWACHA** watishia kuandamana sababu ubunge kina Mdee

UKURASA 16

UKURASA 11

# Mambo 8 waliyoteta Rais Samia, Kenyatta

UKURASA 2




Rais Samia Suluhu Hassan akiwa katika mazungumzo na Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, baada ya kuwasili Ikulu, jijini Nairobi, nchini Kenya jana. **PICHA: IKULU**

# Hivi ndivyo itakavyokuwa mishahara kuanzia Julai

UK.3

# Serikali yafuta penalti mikopo elimu ya juu

UKURASA 2

**MICHEZO** **TUHUMA RUSHWA YANGA, PRISONS BUNGENI** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Mambo manane waliyoteta Rais Samia, Kenyatta

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameanza ziara yake Kenya kwa kukubaliana na mwenyeji wake, Rais Uhuru Kenyatta, mambo anayoyataja yataondoa kwa kiasi kikubwa vikwazo vya kibiashara kati ya nchi zao.

Wakizungumza na waandishi wa habari baada ya kumaliza mazungumzo yaliyowachukua saa tatu, Rais Samia pia alimtangaza Rais Kenyatta kuwa mgeni rasmi wa sherehe za uhuru wa Tanzania Desemba 9, mwaka huu.

Rais Samia aliorodhesha waliyokubaliana katika biashara, uchumi na afya, baadhi kutiwa saini mengi yaligusa kusafisha mazingira ya kibiashara.

Alisema wameafikiana kuielekeza tume ya pamoja nchi hizo mbili kuondoa vikwazo vyote visivyo vya kodi ili kurahisisha nyendo zote za biashara mipakani.

Sambamba na hilo, Rais Samia alisema wamewaelekeza mawaziri wao wa afya kukutana mara moja kuweka mfumo usio na urasimu wala kuchukua muda kuhusiana na ukaguzi unaohusiana na maambukizi ya virusi vya corona, ili kurahisisha biashara.

Lingine, alidokeza kwamba wametia saini makubaliano ya mipango mkakati wa gesi na nishati ya umeme, vivyo hivyo akiwa na maelezo mahsusi kuhusu mradi wa bomba la gesi kati ya Tanzania na Kenya.

Kwa mujibu wa Rais Kenyatta aliyezungumza awali, wamekubaliana kuwekwa bomba la gesi kutoka Dar es Salaam kwenda Kenya bila kutaja mji mahsusi, ili kuvirahisishia viwanda kupata nishati kirahisi. Katika uchumi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), alisema wamekubaliana kuweka mkakati wa pamoja kuwasukuma wanachama wengine wanaolegea kulipa michango.

Wengine wanaounda EAC ni Burundi, Rwanda, Uganda, Sudan Kusini.

Alisema uwekezaji wa Kenya nchini Tanzania, nchi hiyo inashika nafasi ya kwanza kutoka kwa wanachama wa EAC na ya tano kimataifa. Alibainisha kuwa Kenya imewekeza miradi 513 iliyoajiri Watanzania 51,000.

Kuhusu uwekezaji wa Tanzania nchini Kenya, Rais Samia alisema hadi sasa kuna kampuni za Tanzania 30 ambazo zimewekeza shilingi za Kenya bilioni 19.33 na kutoa ajira 2,640.

"Wastani wa biashara kwa miaka mitano kwa nchi mbili ni kati ya shilingi trilioni moja za kitanzania. Nchi zetu bado zina fursa kubwa na Mungu ametupendelea tunakwenda kuzitumia," alisema Rais Samia.

Mbali na kuahidi kuendeleza ushirikiano, Rais Kenyatta alitaja lingine waliloafikiana ni kuanzishwa safari ya mizigo kupitia Ziwa Victoria zitakazojumuisha pia Uganda.

Rais Kenyatta alisema nchi yake kwa sehemu kubwa inapakana na Tanzania ndani ya EAC, hivyo mazungumzo yaligusa kuimarisha usalama kati ya nchi hizo jirani.



Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Pugu Kajiungeni, jijini Dar es Salaam, Dk. Mingole Saidi (kushoto), akiandika maelezo ya mgonjwa, Abedi Abdallah, aliyefika kufanyiwa upasuaji wa busha, wakati wa uzinduzi wa utoaji wa huduma hiyo ya bure ya mwezi mmoja kwa wananchi. Kulia ni Muuguzi Mfawidhi wa kituo hicho, Beatrice Mosha. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Wataka mabadiliko sheria likizo uzazi

**Na Mwandishi Wetu,** SINGIDA

WAKATI wiki iliyopita dunia iliadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi), wanawake walio kwenye utumishi wa umma na sekta binafsi wameiomba serikali kuvifanyia marekebisho baadhi ya vipengele vya Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini ili kutoa haki na kukidhi mahitaji ya kiafya kwa malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto.

Wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti, walisema sheria hiyo imekuwa kikwazo katika utekelezaji wa miongozo, kanuni na taratibu zingine za kiafya.

Wakati miongozo ya afya inataka mtoto mchanga anyonyeshwe maziwa ya mama pekee kwa miezi sita mfululizo bila kumchanganyia chakula kingine, walisema Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini inatoa siku 84 tu za likizo ya uzazi ambazo hazizidi miezi mitatu na hiyo ni hatari kwa afya ya mtoto mchanga.

Neema Omari, mkazi wa Ginnery mjini hapa, alisema kutokana na siku za likizo kuwa chache wanalazimika kukamua maziwa yao na kuyahifadhi kwenye chupa ya chai ili mtoto apewe na yaya au mtu mwingine anayebaki nyumbani pindi mama awapo kazini.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Ernest Mugeta, alisema ingawa mtindo huo umezoeleka kwa kinamama watumishi wanaonyonyesha, njia hiyo si sahihi kwa kuwa mbali na maziwa hayo kupungukiwa baadhi ya virutubisho yanapohamishwa kutoka kwa mama kwenda kwenye chombo kingine, pia inatenganisha uhusiano mwema baina ya mama na mtoto.

Kimsingi, uhusiano wa karibu wa mama na mtoto hutokana na mtoto kunyonyesha titi la mama, anazoea harufu ya mama ndiyo maana mtoto humjua mama zaidi kuliko baba. Inashauriwa pale inapowezekana mama apewe ruhusa ya kwenda kunyonyesha hata baada ya likizo yake ya uzazi kumalizika," alisema.

# Serikali yafuta penalti ya mikopo elimu ya juu

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

SERIKALI imeendelea kusikia kilio cha wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu baada ya jana Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, kutangaza kufuta tozo ya adhabu ya asilimia 10 ambayo inatozwa kwa wanufaika wanaochelewa kuanza kulipa mikopo ya elimu ya juu.

Hatua hiyo imekuja zikiwa zimepita tatu tangu Rais Samia Suluhu Hassan alipotangaza jijini Mwanza kufuta ongezeko la asilimia sita ya mkopo huo kila mwaka ili kulinda thamani ya fedha.

Akiwasilisha bungeni jana makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, Profesa Ndalichako alitangaza kufutwa kwa tozo hiyo ya asilimia 10 kuanzia Julai Mosi mwaka huu.

Profesa Ndalichako alisema: "Katika utekelezaji wa maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani yaliyofanyika kitaifa mkoani Mwanza Mei Mosi mwaka huu, serikali itaondoa tozo ya asilimia sita ya kulinda thamani ya fedha katika urejeshaji wa mkopo kuanzia Julai Mosi mwaka huu iliyokuwa inatozwa kwa wanufaika wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu.

"Vilevile, serikali inaiagiza Bodi ya Wakurugenzi ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) kuondoa pia tozo ya adhabu ya asilimia 10 ya mkopo ambayo inatozwa kwa wanufaika wanaochelewa kulipa mikopo hiyo."

Profesa Ndalichako alibainisha kuwa katika mwaka ujao wa fedha, serikali kupitia HESLB, itaimarisha mifumo ya TEHAMA ili kuwa na mifumo rafiki itakayowezesha ukusanyaji wa Sh. bilioni 200.

Alisema serikali itaanzisha kituo mahsusi cha wateja jijini Dar es Salaam ili kuboresha huduma za bodi ya mikopo kwa wateja hususani katika urejeshaji wa mikopo.

Waziri huyo alisema serikali itasimamia uombaji, uchambuzi na utoaji wa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 500 kwa wanafunzi wahitaji wapatao 148,581.

Alibainisha kuwa kati yao, wanafunzi 50,250 watakuwa wa mwaka wa kwanza na wanaoendelea na masomo 98,331.

Profesa Ndalichako alisema serikali itakamilisha mifumo ya TEHAMA kupitia mradi wa maboresho ya TEHAMA wa HESLB itakayowezesha uunganishwaji wa mifumo ya bodi na ya wadau, ili kurahisisha ubadilishanaji wa taarifa na hivyo kuongeza ufanisi katika kuwahudumia wanafunzi, waajiri na wanufaika wa mikopo.

"Serikali pia itakamilisha tathmini ya namna bora ya kugharamia wahitimu wenye ufaulu wa juu na wale wanaopata ufadhili wa masomo katika vyuo maalum nje ya nchi kusomea fani mahsusi zinazoweza kuchochea ufanisi na kuchangia ukuaji uchumi," alisema.

Profesa Ndalichako pia alisema serikali itafanya mapitio ya viashiria na ving'amuzi vya uhitaji vinavyotumika kupima uhitaji wa mikopo kwa kuzingatia hali za kimaisha kwa lengo la kuboresha utoaji wa mikopo kwa wanufaika.

Alisema serikali itaandaa mpango mkakati wa bodi wa awamu ya tano (2022/23 - 2026/27) utakaolenga kujenga uwezo wa HESLB kuwa himilivu na kujiendesha kama mfuko wa mikopo.

Alisema serikali itaendeleza na kuimarisha ushirikiano na wadau wa kimkakati ili kuwafikia waajiri na wanufaika katika mikoa na wilaya mbalimbali kwa kuendesha programu mahususi za elimu ya uombaji na urejeshaji wa mikopo.

HABARI KITAIFA



Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba (kulia), akiwa katika majadiliano na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya CRDB, Dk. Ally Laay (katikati) na Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Abdulmajid Nsekela, kujadili masuala yanayohusu uendeshaji wa benki hiyo jijini Dar es Salaam jana. **Habari Uk 7**. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Hivi ndivyo mishahara itakavyokuwa Julai

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa, amewataka watendaji na maofisa utumishi kutoa elimu kwa watumishi walio chini yao kuhusu watakavyonufaika na uamuzi wa serikali kupunguza kodi na tozo katika mishahara yao.

Katika ziara yake ya kikazi mkoani Mwanza juzi, Mchengerwa alisema hotuba ya Rais Samia Suluhu Hassan wakati wa sherehe za Mei Mosi mwaka huu, iliainisha wazi azma yake ya kuzifanyia kazi vikwazo vinavyowakabili watumishi wa umma nchini.

Aliwataka watendaji na maofisa utumishi kutoa elimu kwa watumishi walio chini yao juu ya vipaumbele hivyo ili watumishi hao wapate kuelewa kwa ufasaha namna serikali ilivyowaondolea kero zilizokuwa zikiwakabili.

Waziri huyo akitolea mfano wa kipaumbele cha punguzo la asilimia moja ya kodi ya mshahara (PAYE) kwa watumishi wa umma, alisema Rais amewapunguzia mzigo mkubwa watumishi wa umma katika hilo kwa kuwa mtumishi anayepokea mshahara wa Sh. 300,000, punguzo la kodi yake ni takriban Sh. 30,000 ambayo ni sawa na kumwongezea mtumishi wa umma nyongeza ya mshahara wa Sh. 30,000 kwa mwezi.

"Ninatamani sana elimu itolewe kwa watumishi juu ya punguzo hili, ili waone ni kwa kiasi gani Mheshimiwa Rais alivyo na mapenzi mema kwa watumishi wa umma," alisema.

Mchengerwa alisema hotuba ya Rais ni sehemu ya mijadala inayohusu haki na stahili za watumishi wa umma nchini, hivyo hawana budi kumpongeza kwa kuliona hilo na kulitolea maelekezo.

Aliagiza watendaji na maofisa utumishi watekeleze kikamilifu maelekezo hayo ili kuondoa vikwazo vinavyowakabili watumishi wa umma.

Ili kuunga mkono azma ya Rais, Mchengerwa aliwataka watumishi wa umma kuendelea kufanya kazi kwa bidii na uadilifu kwa kuwa tangu aingie madarakani, ni kipindi cha miezi miwili tu amedhamiria kuondoa kabisa kero zinazowakabili watumishi ili kuwajengea ari kiutendaji.

Aliwataka watendaji katika taasisi za umma kutoa ufafanuzi wa vipaumbele vingine vinavyohusu stahiki za watumishi wa umma vilivyoainishwa kwenye hotuba ya Rais kukiwamo kufutwa kwa ongezeko la asilimia sita kila mwaka katika deni la Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) na kuongezeka kwa ukomo wa umri wa watoto kutoka miaka 18-21 kwenye huduma ya bima ya afya.

Akizungumzia suala la upandishwaji wa madaraja, malimbikizo ya madai ya watumishi, maboresho ya miundo ya kiutumishi kwa baadhi ya kada na ajira mpya, Mchengerwa alisema katika kutekeleza vipaumbele vya Rais, serikali imetenga Sh. bilioni 60 kwa ajili ya kulipa madai ya watumishi, Sh. bilioni 499 kwa ajili ya upandishwaji wa madaraja, Sh. bilioni 120 kwa ajili ya kuboresha miundo ya baadhi ya kada na zaidi ya Sh. bilioni 200 kwa ajili ya kuajiri watumishi 40,000 katika sekta za afya, elimu, ardhi na kilimo.

Waziri huyo aliwataka watendaji na maofisa utumishi kuzifanyia kazi kero za kiutumishi wa watumishi walio chini yao, ikiwa ni pamoja na kuwasilisha madai ya watumishi ili yahakikiwe na kulipwa.

Aliahidi kushughulikia kwa wakati mashauri ya kinidhamu ya watumishi wa umma ili kuiondolea serikali mzigo wa kulipa fidia pindi watumishi hao wanapokata rufani Tume ya Utumishi na Uamuzi na kushinda rufani zao.

Kuhusu mafao ya wastaafu, Mchengerwa aliwataka waajiri kuhakikisha wanawasilisha michango ya watumishi wa umma kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii kwa wakati ili wanapostaafu, wapate stahiki zao kwa wakati.

Ziara hiyo Mchengerwa ililenga kutoa ufafanuzi wa vipaumbele katika hotuba ya Rais Samia ya Mei Mosi mwaka huu na kuhimiza utekelezaji wa vipaumbele hivyo kwa watendaji ili kuwawezesha watumishi wa umma kupata stahiki zao kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma.

## Bunge lataka fedha za maji kutoka Misri

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ameitaka Wizara ya Fedha na Mipango kutoa maelezo kuhusu fedha zilizotolewa na Serikali ya Misri kwa ajili ya kuchimba visima virefu 30 vya maji.

Ndugai alitoa kauli hiyo jana bungeni, baada ya kumalizika kujibiwa swali la Wizara ya Maji lililohusu mkopo fedha za India kwa ajili ya miradi ya maji.

Alisema: "Huu ni mkopo usio na riba hii mipango ni miaka miwili imesimama hivyo kalikwamueni kama wako serious kwenye mipango hiyo tujulishwe tuelewe ili tusiwe tunawasumbua pale tulipokuwa tumesaidiwa na tuna shida kubwa namna hii, tatizo ni nini."

Katika swali la msingi, Mbunge wa Handeni (CCM), Reuben Kwagilwa, alihoji serikali lini itatekeleza ahadi yake ya ujenzi wa mradi mkubwa wa maji Handeni Trunk Main (HTM).

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, alisema serikali ilipata mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India kupitia Benki ya Exim ya India jumla ya Dola za Marekani milioni 500 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika miji 28 nchini.

Alisema miongozi mwa miradi hiyo ni wa maji wa Kitaifa Handeni utakaohudumia vijiji 84 katika Wilaya ya Handeni na miji midogo ya Mkata, Komkonga, Kabuku, Michungwani/ Segera na mji wa Handeni.


## VEHICLES SALES

Arysta LifeScience Tanzania is advertising the sale of two company vehicles located in Morogoro and Mbeya. All interested buyers are welcome to view the vehicles at the following locations,

1. Morogoro (Kihonda)
   Type: Nissan
   Model: Hard Body (Double Cabin)
   Color: White
   Mileage: 250,000km

**Contacts:**
**+255 762 748 291; +255 762 535 410**

2. Mbeya-(SAE-Pipeline)
   Type: Nissan
   Model: Hard Body (Double Cabin)
   Color: White
   Mileage: 246,000km

**Contacts:**
**+ 255 767 256 444: +255 762 535 410**

# Lydia Igarabuza: Natamani wanawake wengi viongozi

**Na Romana Mallya**

MENEJA wa Vipindi wa East Africa Radio, Lydia Igarabuza, ameishauri serikali kuanzisha vituo maalum ambavyo vitawezesha wanawake kupata mbinu za kuwajengea uwezo kwenye uongozi.

Lydia alitoa ushauri huo jana wakati wa mahojiano maalum na Nipashe akiwa ni miongoni mwa wanahabari wanawake 25 walioshinda tuzo zilizotolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO).

Tuzo hizo ambazo zilitolewa wiki iliyopita, zililenga wanahabari wanawake viongozi na wanaochipukia ambao wamegusa maisha ya watu wengi, zilitolewa na UNESCO kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Wanahabari Waandamizi wa Kampuni ya IPP wengine walioshinda tuzo hizo ni Mkurugenzi wa ITV Radio One, Joyce Mhavile na Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe.

Lydia alisema utafiti unaonyesha kuwapo wanawake kwenye nafasi za juu za uongozi, huongeza kasi ya maendeleo na kupendekeza kuwekeza kwao kuhamasishwe zaidi.

"Binafsi ninashauri taasisi za uongozi kama ile ya 'Uongozi Institute' tuwe nazo nyingi nchini ili watu wachague waende wapi kupata mafunzo ya uongozi, hii ni njia mojawapo ya kusaidia kuwajengea uwezo wanawake wengi wanaotaka kuwa viongozi hasa sekta binafsi," alisema.

Alisema tuzo hiyo ni ya tatu kupokea, nyingine ni za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) zinazotolewa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) na kushinda katika maeneo ya Uongozi Bora na Kilimo.

Alisema tuzo aliyopewa na UNESCO imetokana na kazi anazozifanya na alizowahi kuzifanya kabla ya kujiunga na East Africa Radio.

Aliwashauri wasichana ambao wanatamani kuwa viongozi siku moja, lazima wahakikishe wanapigania vitu ambavyo anatamani wawe badala ya kusubiri kushikwa mkono.

"Lazima utafute njia, uonyeshe upo tayari usikae tu nyuma, kama upo kazini pigania ulichonacho ili siku moja wale walio juu wakuone kupitia kazi yako unayofanya," alisema.

Lydia ambaye ana miaka 20 kwenye vyombo vya habari alisema alipenda kuwa sehemu ya uongozi ndiyo maana ameweza kukabiliana na matatizo ya kuwa kiongozi.

Alisema ana Shahada ya Uzamili ya Uandishi wa Habari Kimataifa aliyoipata nchini Uingereza baada ya awali kusoma Diploma ya Utangazaji nchini humo.




Meneja wa Vipindi wa East Africa Radio, Lydia Igarabuza. **NA MPIGAPICHA WETU**






# Sera ya elimu, mitaala kufumuliwa

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

SERIKALI inatarajia kufanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, kwa lengo la kuhakikisha kuwa inakidhi mahitaji ya sasa.

Pia itafanya ufuatiliaji na tathmini ya kina ya mitaala inayotumika kwa sasa, ili kuhakikisha kuwa ufundishaji na ujifunzaji unafanyika kwa kuzingatia viwango na vigezo vilivyowekwa.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, aliyasema hayo jana bungeni wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa wizara yake kwa mwaka 2021/22. Prof. Ndalichako pia alisema serikali itafanya mapitio ya Sheria ya Elimu ya mwaka 1978, ili kuhakikisha inaendana na mazingira ya sasa ya utoaji wa elimu nchini.

"Katika mwaka ujao wa fedha 2021/22, Serikali pia itaweka msisitizo zaidi katika ufundishaji wa masomo ya ufundi, kwa kuimarisha mafunzo kwa vitendo katika shule za sekondari za ufundi zilizopo ambazo ni Iyunga, Ifunda, Tanga, Bwiru Wavulana, Musoma, Mwadui, Moshi na Mtwara," alisema Profesa Ndalichako.

Vilevile, Prof. Ndalichako alisema katika mwaka ujao wa fedha serikali itaimarisha ufundishaji wa masomo yanayowajengea wanafunzi ujuzi katika shule za msingi na sekondari. Aliyataja masomo hayo kuwa ni kilimo, ufundi, stadi za kazi, michezo na biashara.

Prof. Ndalichako alisema katika mwaka ujao wa fedha, serikali itafanya ufuatiliaji na tathmini ya kina ya mitaala inayotumika kwa sasa ili kuhakikisha kuwa ufundishaji na ujifunzaji unafanyika kwa kuzingatia viwango na vigezo vilivyowekwa.

Alivitaja vigezo hivyo ni uwiano wa walimu utakaolingana na idadi ya wanafunzi, vitabu na mazingira ya kujifunzia.

Kadhalika, Prof. Ndalichako alisema wizara itafanyia kazi maoni na ushauri wa wadai wa elimu kuhusu utekelezaji wa sheria ya mwaka 2018 iliyounda Bodi ya Kitaalamu ya Walimu. Aliongeza kuwa wizara pia itazingatia pia maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo walioutoa katika majadiliano kuhusu Kanuni za Bodi ya Kitaalamu ya Walimu yaliyofanyika Aprili 28, mwaka huu kati ya Wizara ya Elimu na Kamati hiyo.

Kuhusu uendelezaji wa elimu ya msingi na sekondari, Prof. Ndalichako alisema serikali itafanya ufuatiliaji na tathmini ya uendeshaji na usimamizi wa shule shikizi katika mikoa 15.

Alisema lengo kuu ni kupima matokeo ya ufundishaji na ujifunzaji na kuweka afua stahiki.

# Jafo aonya viwanda uchafuzi mazingira

**Na Mwandishi Wetu**



SERIKALI imesema kamwe haitakuwa kikwazo kwa wawekezaji wanaolenga kuwekeza katika sekta ya viwanda, lakini wazingatie maendeleo ya viwanda ni lazima yaende sambamba na hifadhi ya mazingira.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, alitoa kauli hiyo jana katika ziara ya kikazi ya kukagua uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira katika kiwanda cha saruji cha Diamond na kiwanda cha kutengeneza nondo cha Lodhia Steel vilivyoko wilayani Mkuranga mkoani Pwani.

Katika ziara kwenye kiwanda cha saruji, Waziri Jafo aliliagiza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuwachukulia hatua za kisheria wamiliki wa kiwanda hicho kutokana na malalamiko ya wananchi juu ya uchafuzi wa mazingira kutokana na kukithiri kwa vumbi linalosababishwa na shughuli za uzalishaji wa saruji kiwandani huko.

"Nimekuja hapa kufuatia malalamiko mengi ya wananchi na wakazi wa maeneo haya, wamiliki wa kiwanda hiki wamezima mitambo yote wakijua ninakuja, wamekimbia.

"Hivyo, NEMC chukeni hatua mara moja, watozwe faini na nipate taarifa mapema ofisini," Jafo alisisitiza.

Hata hivyo, Waziri Jafo ameridhishwa na uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 katika Kiwanda cha Lodhia Steels na kuwataka wawekezaji wengine kwenye sekta ya viwanda kuiga mfano wa kiwanda hicho kwa kuhakikisha shughuli za uzalishaji zinafanyika bila kuharibu mazingira na kuhatarisha afya za binadamu na viumbe hai.

"Katika viwanda vyote vinavyofanya shughuli ya uzalishaji wa nondo hapa nchini, kiwanda hiki ni mfano wa kuigwa katika kuhifadhi na kutunza mazingira.

"Pia kimetoa ajira kwa Watanzania wapato 700 na kuzalisha tani 200 za nondo kila siku zenye ukubwa wa milimita 8-40 ambazo zinatumika katika miradi ya kimkakati hapa nchini kama ujenzi wa reli ya kisasa, ujenzi wa bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere pia daraja la Tanzanite," Jafo alisisitiza.

Jafo alionya waharibifu wa miundombinu ya nchi kwa kigezo cha kuuza chuma chakavu na kusisitiza kuwa hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

"Serikali inatumia fedha nyingi katika ujenzi wa miundombinu ya reli na barabara. Baadhi ya watu wanaokoteza mitaani chuma chakavu, tusipokuwa wakali tutatengeneza miundombinu na kuharibu miundombinu pia, lazima tulinde miundombinu ya nchi," alisema.

Mkurugenzi wa Lodhia Steel, Saileth Pandit, aliiomba serikali kufanya mabadiliko ya sera na mikataba ya kimataifa inayozuia uingizwaji wa malighafi ya chuma chakavu kutoka nje ya nchi ili kuwezesha viwanda kupata malighafi za kutosha kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa za chuma nchini.

# RC aanika neema uwekezaji Pwani

**Na Idrisa Sadick**

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Evarist Ndikilo, amewahakikisha wawekezaji uwapo wa ardhi kubwa kwa ajili ya uwekezaji mkoani humo.

Katika mazungumzo yake na wawakilishi Chemba ya Wafanyabiashara wa China nchini, kuhusu uwekezaji wa viwanda jana, mkoa huo tayari ulishatenga ardhi kwa ajili ya uwekezaji huo.

Mazungumzo hayo yalifanyika katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa lengo la kuwapatia ardhi wawekezaji hao ili wajenge viwanda vya kusaidia kukua kwa uchumi wa nchi.

Ndikilo alisema amepokea ugeni huo uliolenga kupata ardhi kwa ajili ya ujenzi wa viwanda ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa maombi waliyowasilisha kwa Rais walipokutana na kufanya mazungumzo hivi karibuni.

"Sisi kama Mkoa wa Pwani suala hili tutalifanyia kazi ili kuwapatia ardhi ya kujenga viwanda," alisema.

Ndikilo aliwaahidi wawakilishi hao kuwa serikali inashirikiana nao bega kwa bega na ilishaandaa maeneo maalum kwa ajili ya ujenzi wa viwanda.

Alibainisha kuwa mkoa huo una eneo la Kwala ambalo litawafaa kwa hekta 500 wanazohitaji kwa ajili ya ujenzi wa viwanda.

Kiongozi huyo wa mkoa alisema eneo hilo ni sahihi kwa uwekezaji kwa kuwa lina miundombinu bora kama vile umeme wa uhakika, maji, barabara, ukaribu wa bandari kavu na reli ya kisasa (SGR).

Wawakilishi hao kwa upande wao wakiongozwa na Janson Huang, alisema wanatarajiwa kujenga viwanda zaidi ya 200 vitakavyozalisha bidhaa mbalimbali ikiwamo dawa, simu za mkononi na viyoyozi.

## MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII TASAF

## UTAMBUZI NA UANDIKISHAJI WA WALENGWA

Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) umeanza zoezi la utambuzi na uandikishaji wa kaya za walengwa wanaokidhi vigezo vya kusaidiwa na Mfuko kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Zoezi hilo litakamilisha utambuzi wa asilimia 30 ya kaya ambazo hazikufikiwa katika kipindi cha Kwanza cha Awamu ya Tatu kilichotekelezwa kuanzia 2013 hadi 2019.

Zoezi la utambuzi na uandikishaji wa walengwa linafanyika kwa awamu na litaendelea hadi mwezi Julai 2021. Mzunguko wa Kwanza umekamilika katika Halmashauri zote za mikoa ya Pwani, Ruvuma, Dodoma, Lindi, Mtwara na Wilaya zote za Unguja na Pemba. Kaya zinazotambuliwa zinahojiwa kupata taarifa zake kwa kujaziwa dodoso. Hatua ya pili ni kuchakata taarifa zilizokusanywa ili kupata kaya zilizokidhi vigezo ambazo zitaandikishwa kwenye daftari la kaya za walengwa.

Mzunguko wa Pili wa utambuzi na uandikishaji wa kaya za walengwa utafanyika mwezi Mei 2021 katika halmashauri zote za mikoa ya Singida, Geita, Mwanza, Simiyu, Kigoma, Katavi na Rukwa. Viongozi wa Vijiji na Mitaa katika maeneo hayo mnatakiwa kuwatangazia na kuwahamasisha wananchi wote katika maeneo husika kuhudhuria mikutano ya utambuzi wa walengwa kwa ratiba itakayopangwa. Zoezi la utambuzi na uandikishaji litafanywa na Timu za wawezeshaji kutoka halmashauri husika na litasimamiwa na Viongozi wa Vijiji na Mitaa. Wajibu wa Viongozi ni kuhakikisha kwamba zoezi la utambuzi linafanywa kwa haki na weledi bila upendeleo au ukiukwaji wa taratibu ili kupata **walengwa wanaokidhi vigezo vilivyowekwa.** Viongozi wa Vijiji/Mitaa/Shehia watakaobainika kuharibu zoezi la utambuzi na kusababisha malalamiko kutoka kwa wananchi, watawajibika katika ngazi zao za usimamizi kwa mujibu wa viapo walivyokula na kutia saini.

Aidha, Wananchi wote mnahimizwa kuhudhuria mikutano hiyo pale itakapoitishwa katika maeneo yenu na kuzingatia maelezo na taratibu zilizowekwa ili kupata orodha sahihi ya watu wanaokidhi vigezo vya kuandikishwa kwenye Mpango wa TASAF.

Idadi ya walengwa kwa Kipindi hiki cha Pili cha Awamu ya Tatu (2020 – 2023) ni Kaya 1,400,000. Walengwa watakaoandikishwa watawezeshwa kujikwamua kiuchumi kwa utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundo mbinu ya elimu, afya na maji kupitia ajira za muda na kuanzisha miradi ya ujasiriamali hivyo kujiongezea kipato.

Ladislaus J. Mwamanga
**MKURUGENZI MTENDAJI**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Pongezi serikali kusikiliza kilio mikopo elimu ya juu

**MWAKA** 1994/95, serikali ilianza kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na miaka 10 baadaye, utoaji wa mikopo hiyo ukachagizwa zaidi na kuanzishwa kwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

Taasisi hiyo yenye umri wa miaka 17, imegeuka kuwa mjadala mkubwa uliochukua sura ya kitaifa; katika mtazamo wa mapitio ya baadhi ya majukumu yake, malalamiko ya namna inavyotoa huduma na kufumuliwa kwa sura na uwajibikaji wake.

Kilio kikuu cha wanufaika wa mikopo hiyo na wadau wa elimu ni kile kilichoitwa 'uonevu' katika makato ya urejeshaji wa mikopo ya bodi hiyo.

Mwongozo wa HESLB katika utoaji wa mikopo umeweka masharti kadhaa likiwamo la deni kuongeza kwa asilimia sita kila mwaka kuanzia tarehe ambayo mnufaika anapokea fedha kwa mara ya kwanza.

Hii ina maana kwamba, kwa mwanafunzi wa taalamu ya udaktari wa binadamu (MD) ambayo huchukua miaka mitano darasani, deni la mnufaika linakuwa limepanda kwa asilimia 30 katika miaka mitano anayokuwa chuoni.

Mei Mosi mwaka huu, katika hotuba yake ya maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani, Rais Samia Suluhu Hassan alitangaza kufuta 'riba' hii iliyolalamikiwa kwa muda mrefu. Mwongozo wa HESLB pia umeweka adhabu ya tozo ya asilimia 10 ya deni pale mnufaika wa mkopo anaposhindwa kuanza kulipa deni baada ya kipindi cha neema cha miezi 24 baada ya kuhitimu masomo yake.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, alitangaza bungeni jana kufuta ongezeko hilo la asilimia 10, alipowasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha.

Nipashe tunaipongeza serikali kwa uamuzi wake wa kufuta tozo hizo kwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu kwa kuzingatia ukweli kwamba kuwapo kwake kuliifanya mikopo hiyo kuonekana ni ya kibiashara badala ya malengo mahususi ya kuanzishwa kwa bodi ambayo ni kusaidia wananchi wanaotoka katika familia duni kiuchumi.

Tunaamini uamuzi huo wa serikali utamaliza tatizo la kutokumalizika kwa deni la mkopo kwa wanufaika walioji-otokeza kukulipa, ikizingatiwa utaratibu wa deni kuongezeka kwa asilimia sita kila mwaka.

Hata hivyo, Nipashe tunaona kuna haja serikali kuzimulika hoja mbili za wadau zilizobaki. Hoja hizo ni pamoja na tozo ya asilimia moja ya deni la mnufaika kwa ajili ya uendeshaji wa bodi ambayo inapewa ruzuku na serikali.

Hoja ya pili ni makato ya asilimia 15 ya mshahara wa mnufaika kila mwezi ambayo yanalalamikiwa kumpunguzia fursa mnufaika kukopeshwa na taasisi zingine za kifedha zikiwamo benki.


Nipashe tunaona kuna haja makato hayo ya asilimia 15 yaliyotokana na marejeo ya mwaka 2016 ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Mwaka 2004 yamulikwe kwa sababu yanasababishwa ukiukwaji wa Sheria ya Maofisa Waliobainishwa (Urejeshwaji wa Madeni) Sheria Na. 7 ya Mwaka 1970.

Sheria hiyo na Mwongozo wenye Kumbukumbu Namba 26/46/01/1/66 wa Novemba 28, 2012, inaweka masharti watumishi wanapaswa kulipwa si chini ya theluthi moja ya mishahara yao ya kila mwezi.

Shime, tunaipongeza serikali kwa kusikia kilio cha wadau katika utendaji wa HESLB. Sasa izigeukie hoja mbili zilizobaki.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Kwa hili, mafunzo ya maadili ni muhimu kwa viongozi hawa

**KULIKONI** Kasesela? Pengine ni kauli za mshangao pengine zilizosikika kutoka kwa wanaotumia mitandao baada ya kurushwa video inayomwonyesha Mkuu wa Wilaya Iringa, Richard Kasesela, akimtukana mmoja wa washiriki wa mkutano aliokuwa akiuhutubia.

Baadaye ikawekwa video nyingine ikimwonyesha mkuu huyo wa wilaya akiomba radhi kutokana na kile alichokifanya na kukiri kuwa yeye kama walivyo binadamu wengine, ambao kimsingi hawajakamilika, alighafilika.

Kitendo cha mkuu huyo wa wilaya kuomba radhi, kinaonyesha ni jinsi gani amejutia kosa alilofanya, hivyo itapendeza iwapo wakazi wa Iringa na Watanzania waliomuona na kumshuhudia watamsamehe.

Lakini kabla ya kuendelea, niseme kuwa hatua alioichukua ya kukiri kosa hilo, ni ya kiungwana, kwani imeonyesha kutambua alichofanya na kukijutia, hivyo si vibaya kumsamehe, kwa kutambua kuwa hakuna binadamu aliyekamilika. Pamoja na hayo, pengine kuna haja ya kuwapo kwa semina elekezi ambayo itawasaidia viongozi wa umma kufanya kazi bila kujiingiza kwenye mmmonyoko wa maadili.

Semina elekezi ni kwa ajili ya kuwasuka viongozi wa serikali yatakayowawezesha kuwaongezea maarifa na stadi za uongozi na utendaji pamoja na masuala ya maadili.

Hiyo ndiyo inayonisukuma kuhimiza kuwapo kwa mafunzo kwa kuwa hata Rais wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, aliwahi kueleza umuhimu wake. Aliwahi kuwaasa wakuu wa wilaya na mikoa wasigeuze matakwa au mapenzi ya mioyo yao kuwa mbadala wa katiba, sheria na kanuni kwani ni kukiuka msingi mkuu wa utawala bora ambao ni kuheshimu utawala wa sheria, huku akiwataka watumie vizuri na kwa hekima madaraka na mamlaka waliyopewa.

**Semina elekezi ni kwa ajili ya kuwasuka viongozi wa serikali yatakayowawezesha kuwaongezea maarifa na stadi za uongozi na utendaji pamoja na masuala ya maadili.**

Katika hotuba aliyotoa akifungua semina elekezi kwa wakuu wa wilaya na mikoa, aliwataka wasiwe waonevu, wasidhulumu, wasiwe wababe, wazuie hasira zao hata pale wanapoudhiwa hata kutukanwa.

Ushauri kama huo leo ungezingatiwa, ungewasaidia kutimiza majukumu yao bila kukwaruzana na wananchi kama ambavyo imetokea huko Iringa hadi kutukana, lakini akumbuke kiongozi wa umma anatakiwa kuwa mfano bora kwa wale anaowaongoza ikiwamo ni pamoja na kuepuka matusi tena hadharani.

Mkuu wa Wilaya ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, vyombo vya ulinzi katika ngazi hiyo viko chini yake, anaweza kuvitumia kuzuia vurugu anapoona kuna mtu anataka kuchafua hali ya hewa sasa naye akiwa ndiye anayeleta vurugu inakuwaje?

Kwa mfano, video ambayo inamwonyesha akitukana ilikuwa ni rahisi kuwaelekeza polisi wamkamate aliyejibizana naye badala ya kutukana hadharani.

Miaka michache iliyopita, Watanzania wameshuhudia jinsi ambavyo baadhi ya wakuu wa wilaya na mikoa walivyokuwa wakiwaswekwa ndani wanasiasa na watumishi wengine wa umma, huku ukamataji huo ukiibua maswali mengi.

Ujumbe muhimu wa kukumbuka ni kuwa ulimi ni kiungo kidogo, lakini unaweza kusababisha madhara makubwa iwapo hautatumiwa kwa umakini, kwa kuwa unaweza kumwingiza mtu katika matatizo bila yeye kutarajia iwapo hatakuwa mwangalifu.

## HABARI KITAIFA

# Vigogo CRDB, Hazina wateta

**Christina Mwakangale**

BODI ya Benki ya CRDB ikiongozwa na Mwenyekiti wake, Dk. Ally Laay na Mkurugenzi Mtendaji, Abdulmajid Nsekela, imekutana na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, kujadili masuala yanayohusu uendeshaji wa benki hiyo.

Mkutano huo ulifanyika katika ofisi ya wizara hiyo, jijini Dodoma na kuhudhuriwa na wajumbe wa bodi wa CRDB, wakurugenzi na maofisa waandamizi.

Akizungumza katika mkutano huo Dk. Laay alimpongeza katibu mkuu huyo kwa kuteuliwa kushika nafasi hiyo, huku akiahidi kutoa ushirikiano wa dhati katika utendaji wake.

Alisema serikali ni sehemu ya wanahisa wa benki hiyo, kupitia Mfuko wa Uwekezaji wa DANIDA ambao Katibu Mkuu huyo ni mwenyekiti wake.

"Tumefika hapa kukusalimia na kukupongeza, lakini kukupa taarifa juu ya masuala mbalimbali ya utendaji wa benki na mabadiliko ambayo tunatarajia kufanya katika katiba ya kampuni tunapoelekea katika mkutano mkuu wa wanahisa utakaofanyika Mei 22, mwaka huu, jijini Arusha," alisema Dk. Laay.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Nsekela, alimweleza katibu mkuu, kuhusu mafanikio ambayo benki imeyapata kwa mwaka wa fedha ulioisha na kwamba faida ilikuwa kutoka shilingi bilioni 175 mwaka 2019 hadi kufikia shilingi bilioni 236 mwaka jana, sawa na ongezeko la asilimia 35.



Meya wa Jiji la Mbeya, Dormohamed Issa Rahmat (katikati), akikata utepe kuzindua ofisi mpya ya kampuni ya D Light, katika Mtaa Lupa jijini humo jana, inayojihusisha na uzalishaji na uuzaji vifaa vya umeme wa jua. Kushoto ni Meneja wa Biashara wa kampuni hiyo, Kanda ya Kusini, Lilian Mwalongo, (wa pili kulia) ni Mwanasheria wa Jiji hilo, Triphonia Kisiga na (kulia) ni Mkuu wa Kitengo cha Ufundi D Light, Prisca Kalinga. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Watu binafsi, watumishi kunufaika mikopo ya simu

**Na Beatrice Shayo**

WANANCHI na watumishi wa umma wataanza kukopeshwa simu kwa gharama nafuu, lengo ni kumwezesha kila mmoja kuingia katika dunia ya kidijitali.

Hayo yalisemwa jijini Dar es Salaam na Meneja wa Mauzo wa kampuni ya Vivo, Simon Noel, wakati wa uzinduzi wa ushirikiano wa kampuni yake na Laina Finance Ltd kwa ajili ya kuanza kutoa simu kwa mkopo wenye masharti nafuu.

Alisema kuna watu wengi wamekuwa wakihitaji simu janja za mkononi (Smart phone) na kujikuta hawana uwezo wa kununua, hali ambayo wameona ni vizuri kuwasaidia ili walipe kidogo.

Noel alisema simu hizo watazitoa kwa makundi mawili ya watumishi wa umma watu binafsi.

Alisema simu hizo kwa watumishi, watatakiwa kulipa kiasi kidogo cha fedha na kupatiwa, na kwamba ndani ya miezi sita atatakiwa awe amekamilisha deni lake.

"Kwa mtu binafsi atatakiwa kulipa kiasi kidogo cha fedha na simu tunampatia, huku akiendelea kulipa kidogo kidogo hadi atakapokamilisha katika kipindi cha miezi mitatu," alisema.

Aliongeza: "Sisi tumekuja kivingine hata kama hujamaliza kulipa tunakupatia simu na utaendelea kutulipa kidogo kidogo kwa muda ambao tumekupatia na hii huduma inatolewa kwa mawakala wote wa nchini, na simu zetu hazina gharama kubwa," alisema.

Noel alisema huu ni wakati wa kutumia simu janja zenye ubora na sio wananchi kuuziwa simu ambazo zipo chini ya ubora na kujikuta wakitumia gharama kubwa katika kuzitengeneza.

Meneja Mkuu wa Laina Finance LTd, Mrisho Shomari, alisema kampuni yake imekuwa ikitoa mikopo, na kwamba wamekubaliana na kampuni ya Vivo kutoa bidhaa hiyo kwa gharama nafuu ili kuwafikia wananchi wengi zaidi.

Alisema wataangalia vigezo vya waombaji kabla ya kuwapatia simu hizo na lengo lao kubwa ni kuleta mapinduzi sokoni ili wananchi wafaidike na ulimwengu wa kidigitali.

# Serikali, sekta binafsi kuinua TEHAMA

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeahidi kushirikiana kwa karibu sana na sekta binafsi kuinua sekta ya TEHAMA na imewaalika wawekezaji kuwekeza katika sekta hiyo ili istawi na wawekezaji nao wanufaike.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia, Dk. Faustine Ndugulile na kwamba serikali imedhamiria kushirikiana na sekta binafsi kuinua sekta ya TEHAMA kwa kuzifanyia kazi changamoto lengo likiwa ni kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji katika sekta hiyo.

"Niseme wazi kabisa, katika nchi yetu kuna idadi kubwa ya kampuni binafsi zinazojihusisha na teknolojia ya mawasiliano na habari, na hii ni ishara nzuri kwetu kwamba sekta binafsi imekuwa mstari wa mbele kujenga sekta hii. Hivyo ninawaahidi kwa niaba ya wizara tutashirikiana kuinua sekta hii ya TEHAMA," alisema waziri na kuongeza kwamba serikali inazitambua changamoto zinazowakabili wadau wa sekta hiyo, na kwamba serikali imedhamiria kuzitatua changamoto hizo.

"Ninachukua fursa hii kuwaalika wadau mbalimbali kuja kuwekeza kwenye sekta ya TEHAMA kwa maana huku pia kuna fursa ambayo inaweza kuwapatia faida kubwa," alisema Dk. Ndugulile.

Waziri alitoa hadi hiyo kufuatia maoni na hoja za wadau wa sekta hii wakati wa mkutano wao wa hivi karibuni jijini Dar es Salaam. Waziri amesema maoni ya wajumbe wa mkutano huo serikali itayafanyia kazi.

Dk. Ndugulile amesema serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa dhati imeonyesha nia ya kushirikiana na sekta binafsi, hivyo changamoto hizi zitafanyiwa kazi ili kuongeza ufanisi kwenye sekta ya TEHAMA.

Katika mkutano huo, Katibu Mtendaji wa Baraza la Biashara la Taifa, Dk. Godwill Wanga, alisema lengo la serikali ni kuhakikisha huduma ya mtandao inapatikana nchi nzima ili sekta binafsi ifanye kazi kwa ufanisi.

"Sekta hii ina faida kubwa kwa ustawi wa sekta binafsi pia hasa wafanyabiashara na kwa vile tumehakikishiwa upatikanaji wa mtandao kwenye maeneo mengi. Hii sasa ikawe fursa kwa wadau kujiingizia kipato na hata kuliingizia pato taifa," aliwaambia wajumbe wa mkutano huo.




# MUCE yaja na mwarobaini wa sumu kuvu

**Na Zuhura Zukheir,** IRINGA

WATAFITI wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE) cha mjini Iringa, wamegundua dawa ya kuzuia sumu kuvu kwenye mazao ya nafaka.

Dawa hiyo inatokana na miti shamba, ugunduzi unaotajwa kuleta suluhisho katika uhifadhi wa mazao hayo.

Akizungumza katika maonyesho ya sita ya utafiti Dk. Juma Mongoyo ambaye ni Mkuu wa Idara wa Kemia katika chuo hicho, alisema walifanya utafiti kupitia mmea aina ya Diospyros Mafiensis, ambao uligunduliwa Mafia ambapo walitumia mizizi yake katika utafiti na kuleta matokeo chanya ya utafiti huo.

Mongoyo alisema katika utafiti wa mmea huo wamebaini mizizi yake hufanya kazi ya kupunguza uzalishaji wa sumu kuvu na kulinda nafaka isishambuliwe na fangasi aina ya Asperigillus flavus na Asperigillus Parasiticus wanaozalisha sumu kuvu kutokana na joto kali na unyevunyevu unaotengeneza fangasi hao.

Dt. Mongoyo alisema kuwa takwimu zinaonyesha kuwa takribani ya watu milioni 4.5 duniani wanakula sumu kuvu kwa kiwango tofauti, ambapo huchukua miaka 30 hadi kujitokeza madhara yake, huku akisema kuwa takwimu huonyesha takribani watu 155,000 hupoteza maisha kila mwaka duniani, kutokana na tatizo la saratani ya maini inayosababishwa na ulaji wa sumu kuvu.

Alisema mizizi ya mmea wa diospyros mafiensis unauwezo wa kulinda nafaka na jamii yote inayoweza kushambuliwa na fangasi hao wajulikanao kama Asperigillus Flavus na Asperigillus Parasiticus

Mgeni rasmi katika uzinduzi huo, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Prof. Yunus Mgaya, alisema NIMR imeona ipo haja ya kushirikiana na MUCE kutokana na utafiti huo wanaoufanya kuwa na lengo moja na NIMR la kulinda afya ya binadamu.

Aidha, profesa Yunus Mgaya aliongeza kuwa katika kuboresha tiba nchini, NIMR inajenga kiwanda cha kuzalisha dawa za asili zitokanazo na mimea ambazo zitakuwa kwa mfumo wa vidonge na unga tofauti na sasa ambapo dawa nyingi za asili ni za maji.




Wafanyakazi wa kampuni za Barrick GoldCorporation na Twiga Minerals Corporation, wakiwa katika maandamano ya maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi), katika Uwanja wa CCM Kirumba, jijini Mwanza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# BAWACHA yawajia juu kina Mdee

**Na Maulid Mmbaga**

BARAZA la Wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA), limesema kuwa wabunge wa viti maalum 19 hawatambuliki kama wanachama CHADEMA), kutokana na ubinafsi na ukaidi wa katiba ya chama hicho.

Hayo yalisemwa na mjumbe wa Kamati Kuu, Suzan Kiwanga jana kwenye ofisi za makao makuu Kinondoni, mkoani Dar es Salaam wakati akiwasilisha taarifa ya BAWACHA, ambapo alieleza kuwa wabunge hao 19 wanashiriki vikao vya bunge kinyume cha katiba.

Alisema kukata rufani kwa waliokuwa wanachama hao hakutengui maamuzi ya awali yaliyotolewa dhidi yao, hivyo kitendo cha Spika wa Bunge, Job Ndugai, kutochukua hatua kwa kuwa kuna rufani alidai kuwa kinaonyesha nia ovu juu ya suala hilo kwani anaelewa taratibu zilivyo.

"Kamati Kuu hatujawahi kupitisha hayo majina ya wabunge 19 wa CHADEMA, chama kina katiba yake, kanuni na miongozo kuhusu vikao vya uendeshaji wa chama, kwa muktadha huo mkutano wa Baraza Kuu ambao utapitia rufani iliyokatwa utakaa kwa mujibu wa katiba ya chama kwa ajili ya kulijadili hilo," alisema.

Alimtaka Spika Ndugai kutekeleza matakwa ya katiba bila masharti kwa kuwa wabunge hao wa viti maalum wanaokaa bungeni kwa mwamvuli wa CHADEMA walivunja katiba ya chama hicho na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivyo si halali kuhudhuria bungeni.

Aidha, alizitaka kamati za utendaji za BAWACHA kila jimbo kukutana na kukaa vikao kwa ajili ya kujadili hatua stahiki za kuchukua dhidi ya suala hilo, na kwamba hawatokuwa tayari kuona katiba ya nchi na ya chama hicho ikivunja.

"Baada ya kupokea mapendekezo kutoka katika majimbo tutatoa maazimio na hatua stahiki tutakazozichukua kwa ajili ya kushinikiza utekelezaji wa jambo hili," alisema Kiwanga.

# Wanahabari wakumbushwa habari za manufaa kwa umma

**Na Beatrice Moses**

WAANDISHI wa habari wametakiwa kuendelea kuandika habari zenye manufaa kwa umma, zikiwamo zinazoibua vitendo vya rushwa vinavyofanywa katika maeneo tofauti, ili kuwezesha hatua za kisheria kuchukuliwa dhidi ya wahusika.

Hayo yamebainishwa juzi na Kamanda wa Kikosi cha Kupambana na Kuzuia Rushwa Wilaya ya Ilala, mkoani Dar es Salaam, Christopher Mwiyava, alipokuwa akizungumza kwenye mkutano wa wadau wa habari ulioandaliwa na Klabu ya Waandishi wa Habari Dar es Salaam (DCPC) kuadhimisha Siku ya Uhuru wa Habari Duniani.

Mwiyava alisema ni jukumu la vyombo vya habari kuanzisha mijadala yenye manufaa kwa jamii na nchi kwa ujumla, kama vile mapambano dhidi ya rushwa.

"Siyo vyema mwandishi kuandika habari kwa upendeleo, kuweka mianya ya rushwa na kutokuwa wazalendo, epuka kuwa tegemezi na kuandika habari zenye maslahi yao binafsi," alisema.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Ilala, Charangwa Suleiman, aliwasisitiza waandishi kuandika habari kwa kuangalia maadili ya kazi yao ikiwamo kuhakikisha wanazungumza na pande zote mbili ili kupata ukweli wa habari husika.

Charangwa aliyasema hayo alipomwakilisha mgeni rasmi Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, ambapo alibainisha kuwa habari zisizozingatia mizani zimesababisha manung'uniko kutoka kwa baadhi ya watu ambao wamekuwa wakituhumiwa kwa jambo fulani, lakini hawakuhojiwa badala yake wanaona habari zinazowahumiza zimetoka kwenye vyombo husika.

"Kwa upande wenu waandishi wapo wasiofuata maadili ya kuandika habari, hali ambayo huzua maswali mengi wanaoisoma ama kuisikia hiyo habari husika, ni vyema kubalance habari kabla haijatoka," alisema.

Mwenyekiti wa DCPC, Irene Mark, alieleza kuwa waandishi wamekuwa wakikabiliwa na vikwazo kadhaa wakiwa katika utekelezaji wa kazi zao, hali ambayo alisema ni kunyima jamii kupata habari husika.

"Waandishi wanaandika habari kwa manufaa ya umma sasa wanapokumbana na vikwazo ni wazi kuwa ni vizuizi habari zisifikwe kwa walengwa ambao ni wananchi, tunashukuru Rais Samia Suluhu Hassan hivi karibuni aliruhusu vyombo vilivyofungiwa kufunguliwa," alisema.

Aibainisha kuwa hata hivvo, kuna hali ya kusuasua katika kuviachia baadhi ya vyombo, hivyo DCPC imewasihi wahusika kufanya mchakato wa kuvifungulia vyombo hivyo ili viweze kufanya kazi ya kuhabarisha umma.

HABARI KITAIFA

# TAMWA yazoa tuzo 15 maadhimisho Uhuru wa Habari

**Na Elizabeth Zaya**

WANACHAMA 15 wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), wamepata tuzo katika maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Habari Duniani.

Tuzo hizo zilitolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kwa wanawake waliofanya kazi za kipekee katika tasnia ya habari na masuala ya jinsia.

Kwa mujibu wa UNESCO, tuzo hizo 15 zilitolewa kwa lengo la kutambua juhudi za wanahabari wanawake nchini katika kuhudumia jamii na kufikia mafanikio makubwa kutokana na uthubutu wa utendaji wao katika tasnia hiyo ya habari nchini.

Wanachama wa TAMWA waliopata tuzo hizo ni pamoja na Mhariri Mtendaji wa gazeti hili, Beatrice Bandawe, Fatma Alloo ambaye ni miongoni mwa waasisi wa chama hicho na mwanzilishi wa Tamasha la Filamu Zanzibar (ZIFF) na Edda Sanga, mwasisi wa TAMWA na mtangazaji wa kwanza wa habari wa kike wa Redio Tanzania huduma ya nje ambaye amechangia katika kuwasaidia kitaaluma mamia ya waandishi wa habari wa kike nchini.

**Tunaishukuru UNESCO na wadau wengine wa habari kwa kutambua mchango wa wanawake hawa ambao wamekuwa chachu ya mabadiliko katika tasnia ya habari.**

Mwanachama mwingine wa chama hicho aliyepata tuzo hizo ni Rose Mwalimu, mwanzilishi wa chama hicho na mwanzilishi mshauri wa redio za jamii nchini na mtetezi wa haki za wanawake kupitia vyombo vya habari.

Wengine ni waandishi waandamizi wakongwe na wahariri katika sekta ya habari, Pili Mtambalike, Valerie Msoka, Evodia Ndonde, Jane Shirima, Halima Shariff, Dk. Joyce Bazira, Penzi Nyamungumi, Irene Bwire, Lilian Timbuka, Assumpta Masoi na Maria Shaba.

"TAMWA tumepokea tuzo hizi kwa heshima kwa sababu wanachama hawa wameonyesha mchango na mabadiliko makubwa katika nyanja ya masuala ya jinsia na katika tasnia hii ya habari," alisema Rose Reuben, Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA.

"Tunaishukuru UNESCO na wadau wengine wa habari kwa kutambua mchango wa wanawake hawa ambao wamekuwa chachu ya mabadiliko katika tasnia ya habari," Reuben.

Mmoja wa wanachama walionyakua tuzo hizo, Lilian Timbuka alisema tuzo hizo zinawahamasisha wanachama hao kuendelea kutoa mchango wao zaidi nchini na kwa kujiamini kupitia tasnia hiyo.



Katibu Tawala wa Mkoa wa Mara, Caroline Albert Mthapula (wapili kulia) akiwa na watumishi wa PPRA; Kulia ni Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi- Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Mara, Timon Kimaro. **MPIGAPICHA WETU**

# MSD yaanza kutengeneza dawa zake

**Na Joseph Mwendapole**

BOHARI Kuu ya Dawa (MSD), imeanza kutengeneza aina kumi za dawa kwa kutumia wataalamu wake, zikiwa ni jitihada za kupunguza utegemezi wa kuagiza dawa nje ya nchi.

Akizunguza na Nipashe jana, Mkurugenzi Mkuu wa MSD, Meja Jenerali Gabriel Mhdize, alisema wameanza na dawa ambazo mahitaji yake ni makubwa lakini baadaye wataongeza zaidi.

Alisema MSD inaagiza aina 606 ya dawa vikiwamo vifaa tiba na vitendanishi vya maabara kutoka nje ya nchi hivyo kuamua kuanza kutengeneza kupunguza mzigo wa kuziagiza kutoka nje.

Alisema wameingia ubia na Kiwanda cha Keko Pharmaceticals Limited ambapo MSD inatumia wataalamu wake yenyewe kutengeneza dawa hizo kiwandani hapo.

Alisema kati ya aina hizo 10 za dawa wanazotengeneza, aina mbili ni za maumivu wakati nane ni za tiba (antibiotics), na kwamba wamezingatia kuanza na hizo kwa sababu mahitaji yake ni makubwa sana.

Alisema MSD ina majukumu matatu ya kununua, kutunza na kusambaza dawa, lakini wanatarajia mabadiliko ya sheria ambayo yatawaongezea jukumu la nne la kutengeneza dawa.

Alisema kwa sasa MSD kwa asilimia 90 inaagiza dawa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara kutoka nje ya nchi.

Meja Jenerali Mhdize alisema alipoingia alianzisha mchakato wa kuwatumia wataalamu wa bohari hiyo kutengeneza dawa na vifaa tiba.

Alisema aliwataka wataalamu wake kila mmoja aandae andiko la nini anaweza kufanya kwa jili ya kuisaidia nchi kwenye eneo hilo na wengi walioandika wameonyesha mafanikio makubwa.

Alisema mwaka jana walianza kutengeneza wenyewe vitakasa mikono na baadaye wakaanza kutengeneza barakoa ambavyo vyote vimepitishwa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA).

Alisema kwa kuanzia mtambo wao ulikuwa na uwezo wa kuzalisha barakoa 45,000 kwa siku, lakini mtambo mwingine utakaposimikwa na kuanza uzalishaji watamudu kuzalisha barakoa 100,000 zingine kwa siku hivyo kufikisha 145,000.

Alisema bado MSD inamaandiko mengi ya wataalamu wake kwenye masuala mbalimbali, ambayo yatafanyiwa kazi siku za mbele kwa ajili ya kulisaidia taifa.

## Wafanyakazi Benki I&M wajitolea damu

**Na Elizabeth Zaya**

ZAIDI ya wafanyakazi 30 wa Benki ya I&M Tanzania wamefanya kampeni ya utoaji damu kama jitihada za kurudisha kwa jamii sehemu ya faida inayopatikana kwenye huduma zake.

Meneja Masoko na Mawasiliano wa Benki hiyo, Anitha Pallangyo, alisema lengo ni kuwezesha serikali kupitia Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, kuwa na akiba ya kutosha ya damu hiyo.

"Kama sehemu ya wananchi na kwa kutambua kwamba damu bado inahitajika kwa ajili ya kusaidia Watanzania wenzetu, benki yetu kupitia mpango wake wa 'IM FOR YOU' ambao wafanyakazi wake hujitolea kwa jamii, tuliamua kufanya kampeni hii ya uchangiaji damu kama njia ya kurudisha kwa jamii," alisema Pallangyo.

"Tumefurahishwa sana na mwitikio ambao wafanyakazi wenzetu wameonyesha katika hili. Tunawashukuru Hospitali ya Muhimbili kwa mwitikio wao walioonyesha kukubali kushirikiana nasi katika hili la utoaji damu ili kuokoa maisha ya Watanzania wengi wenye uhitaji wa damu."

Meneja Mkuu wa kitengo cha uboreshaji huduma za benki hiyo, Deepali Ramaiya, alisema mpango huo ni miongoni mwa ambayo imekuwa ikianzishwa au kubuniwa na wafanyakazi wenyewe wa benki hiyo.

## Tiba mbadala, asili wapewa masharti

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAGANGA wa tiba asili na tiba mbadala wametakiwa kusalimisha nyara za serikali za kurithi wanazomiliki ili wapatiwe vibali vya umiliki wake.

Kauli hiyo ilitolewa mkoani Shinyanga na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Elias Kwandikwa, wakati wa mkutano wa hadhara katika Kata ya Uyogo, Halmashauri ya Ushetu akiwa anasikiliza na kutatua kero za wananchi wa jimbo lake.

Kwandikwa ambaye ni mbunge wa Ushetu mkoani Shinyanga, alisema kuendelea kumiliki nyara hizo ni kosa kwa mujibu wa sheria, hivyo wanatakiwa kuzisalimisha serikalini ili kutambuliwa na kupatiwa vibali maalumu kwa ajili ya shughuli za tiba.

"Mimi niko tayari kuwasaidia kupata vibali serikalini kwa ajili ya kumiliki nyara hizo, mnachotakiwa kukifanya ni kujisajili kwenye mamlaka za serikali," alisema Kwandikwa.

# Eneo la umwagiliaji lafikia hekta 695,045

Kutoka Bungeni DODOMA

Habari na Augusta Njoji

BUNGE limeelezwa kuwa katika kipindi cha mwaka 2019/20 na 2020/21 eneo la kilimo cha umwagiliaji limeongezeka na kufikia hekta 695,045.

Hatua hiyo imechangia kufikia asilimia 58 ya lengo la kufikia hekta milioni 1.2 ifikapo 2025.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Agnesta Kaiza.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali ina mkakati gani wa kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji katika mikoa ya Kigoma, Mwanza, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma na Morogoro ili kuongeza mazao ya kilimo yatakayosafirishwa kupitia reli ya kisasa (SGR).

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Bashe alisema ongezeko hilo limetokana na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu ya Kilangali Seed Farm (Kilosa) kupitia mradi wa ERPP na skimu 13 za SSIDP kupitia mradi wa SSIDP.

**Kwa sasa inaendelea kuandaa mpango utakaoruhusu maduka makubwa ya dawa kutoa huduma hiyo kwa wananchi wanaotumia bima ya afya.**

Alisema serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea kutekeleza kilimo cha umwagiliaji katika mikoa inayopitiwa na SGR kuanzia Mkoa wa Dar es Salaam, Mwanza, Tabora na Kigoma ili kutathmini maeneo yote ya uzalishaji na kuhakikisha kuwa miundombinu sahihi inajengwa katika maeneo hayo.

"Ili SGR itakapokamilika iweze kutumika katika kusafirisha mazao ya kilimo. Serikali imekamilisha ujenzi wa awali kwa skimu za umwagiliaji ya Nyida (Shinyanga), Mwalunili (Igunga), Gwanumpu (Kakonko), Itagata (Singida), Mvumi na Kilangali (Kilosa), Dakawa na Kigugu (Mvomero) na Msolwa ujamaa na Njage (Kilombero)," alisema.

Aidha, alisema serikali itaendelea na ukamilishaji wa skimu hizo ili kutumika ipasavyo na wakulima.

"Kwa sasa serikali inakamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa mradi wa Luiche (Ujiji/Kigoma) wenye hekta 3,000 ambapo ujenzi wa mradi huo unatarajiwa kuanza katika mwaka wa Fedha 2021/22," alisema.

Vilevile, alisema miradi mingine ya umwagiliaji inayopitiwa na SGR itakayotekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 ni pamoja na skimu ya Ngomai (Kongwa), skimu za Nata na Idudumo (Nzega), skimu ya Msufini pamoja na Shamba la Mbegu la Msimba (Morogoro).



Mbunge Viti Maalumu (CCM), Najma Murtaza Giga, akizungumza Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Ahadi za viongozi wakuu wa nchi zawekewa mkakati

SERIKALI inatarajia kuja na mkakati wa kuhakikisha inatekeleza ahadi za viongozi wakuu wa nchi kwa vitendo.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, alibainisha hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Nkasi Kaskazini CHADEMA), Aida Khenani.

Katika swali lake, Mbunge huyo alitaka kujua ni lini serikali itakamilisha ujenzi wa barabara iliyoahidiwa na Hayati John Magufuli katika jimbo lake.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Silinde alisema ofisi hiyo inakuja na mikakati ya kuhakikisha ahadi za viongozi zinatekelezwa na kusisitiza kuwa ahadi hizo zitatekelezwa kwa vitendo.

"Serikali imeendelea kujenga miundombinu ya barabara na kufanya matengenezo katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Mtwara Mjini (CCM), Hassan Mtenga alitaka kujua mpango wa serikali wa kujenga barabara za lami katika Kata za Ufukoni, Magomeni na Shangani katika Manispaa ya Mtwara Mikindani.

Akijibu swali hilo, Silinde alisema katika mwaka wa fedha 2017/18 kupitia Miradi ya Uendelezaji Miji Serikali ilijenga barabara za lami zenye urefu wa kilomita 4.53 katika kata ya Shangani Manispaa Mtwara Mikindani kwa gharama ya Sh. bilioni 7.09.

Hata hivyo, alisema katika mwaka wa fedha 2019/20 kupitia fedha za mfuko wa barabara, serikali imejenga barabara za lami zenye urefu wa kilomita 0.85 katika kata ya Shangani kwa gharama ya Sh. milioni 232.98.

Alibainisha katika mwaka wa fedha 2020/21 barabara zenye urefu wa kilomita 22.37 zimefanyiwa matengenezo na kilomita 1.3 zinaendelea na matengenezo kwa gharama ya Sh. milioni 74.19 katika kata za Ufukoni na Magomeni.

Pia alisema serikali inatambua ukuaji wa haraka wa Mji wa Mtwara na itaendelea kuupa kipaumbele cha barabara za lami na mifereji ya maji ya mvua kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

# Uwiano wa miaka elimu ya msingi Zanzibar, Bara waja

WIZARA ya Elimu, Sayansi, Teknolojia imesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inafanya mapitio ya sera ya elimu ili kuweka uwiano wa miaka kwa elimu ya msingi kati ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Omar Kipanga, alitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Najma Murtaza Giga.

Katika swali la mbunge huyo, alihoji serikali haioni umuhimu wa kuwa na sera na mitaala shirikishi ili kuwa na msingi wa aina moja kuanzia elimu ya maandalizi, elimu msingi na sekondari kati ya Tanzania Bara na Zanzibar ili kuongeza ufaulu zaidi kwa upande wa Zanzibar.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kipanga alisema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikishirikiana vizuri na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala mbalimbali ikiwamo suala la elimu hususan katika utekelezaji wa mitaala na kutoa elimu bora kwa watoto wa Kitanzania.

"Kuhusu sera na mitaala shirikishi baina ya pande mbili za Muungano, Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) hushirikiana na Taasisi ya Elimu Zanzibar (TEZ) katika masuala mbalimbali yahusuyo utekelezaji wa mitaala," alisema.

Alibainisha kuwa ushirikiano huo hutoa fursa mbalimbali ikiwamo mijadala kuhusu utekelezaji wa mitaala na jinsi ya kukabiliana na kero mbalimbali zitokanazo na ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi.

Alitoa rai kwa Watanzania wote kutumia nafasi hiyo ili kutoa maoni yao kuhusu mfumo huo.

## JAMILA BORAFYA:

Wawakilishi sikilizeni jambo linalokwaza wenye ulemavu

Ukurasa 13





Ukurasa 14

## THOMAS SANKARA, PAT LUMUMBA:

siasa

JUMATANO MEI 5, 2021


Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

UCHAMBUZI

# Mbatia vs Awamu ya Sita

## ■ Aionyesha ilipo katiba mpya
## ■ Maeneo korofi kwa wapinzani



James Mbatia.

**Na Christina Mwakangale**

WAKATI vuguvugu la kutaka awamu ya sita ifanikishe mchakato wa Tanzania kupata katiba mpya, Chama cha NCCR-Mageuzi kinapendekeza kurejewa kwa rasimu ya Warioba kwa maelezo kuwa ndilo andiko, lililotokana na matakwa ya wananchi.

Aidha, inatajwa kuwa ni rasimu iliyopatikana kwa kufuata mchakato wa kupata maoni ya umma ya namna katiba mpya wanavyotaka iwe na ndicho kigezo cha chama hicho kusimamia msimamo huo.

Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi, James Mbatia, anasema na kukumbusha kuwa kuna nakala tatu za katiba, ikiwamo inayotumika sasa -Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Rasimu ya Jaji Warioba ya mwaka 2014 pamoja na Katiba Pendekezwa iliyotokana na Bunge Maalumu la Katiba.

Mbatia anayasema hayo katika mahojiano maalumu na Nipashe jijini Dar es Salaam, kuhusu masuala mbalimbali ikiwamo hali ya siasa nchini na kukumbusha kuwa kuna uhitaji mkubwa wa katiba mpya kwa sababu, unatajwa na Watanzania wengi hivi sasa.

"Hata kama andiko tulilonalo sasa lina upungufu na kufanyiwa marekebisho takribani 14, bado ndiyo katiba iliyopo iheshimiwe, lakini kuwe na maandalizi ili kuipata mpya ambayo itakidhi matakwa ya muda tulio nao," anasema Mbatia.

### KASORO ZILIZOIBUKA

"Katiba ya sasa inatoa haki lakini ina mapungufu mengi na bado ipo katika mfumo wa chama kimoja na inaendelea kuutukuza."

Mbatia anautaja uamuzi wa awamu ya nne, kuanzisha mchakato wa upatikanaji katiba mpya kuwa wa kupongezwa, ingawa wananchi ndiyo walipaswa kufanya maamuzi hayo.

Anafafanua kwamba mchakato wa upatikanaji katiba mpya ulioanzishwa mwaka 2013 na kisha kupatikana iliyopendekezwa bungeni, haukuwa na utaratibu wa kuwashirikisha wananchi.

"Katiba ni mama, bunge, mahakama, serikali ni mtoto, na rais yupo ndani ya katiba, kuanzisha mchakato huo, wakati hivi nilivyotaja haitegemewi kuwa na katiba ya wananchi, vyanzo hivi haviwezi kuzaa katiba mpya," anasema Mbatia na kuongeza...

"Udhaifu wa mfumo wetu ulifanya rais aanzishe mchakato huo, lakini bado ilitakiwa uanzishwe na wananchi sababu ndiyo wenye hitaji na mamlaka."

Anaongeza zaidi: "Katiba iliyotokana na wananchi ni rasimu ya mabadiliko ya katiba, iliyoandaliwa na Jaji Warioba mwaka 2014."

Mbatia anasema chama chake kinaitazama rasimu hiyo na ikirejewa sasa inakuwa ni katiba ambayo inayotokana na wananchi, kwa vile kuandaliwa kwake kulihusisha maoni ya Watanzania Bara na Wazanzibari.

Anasema yaliyomo kwenye katiba ya sasa ya mwaka 1977, pamoja na kufanyiwa marekebisho kadhaa, bado yanaminya demokrasia na uwanja usio sawa wa kisiasa.

"Katiba inatoa haki ya kisiasa kwa vyama vya siasa lakini wakati huohuo serikali ilifikia hatua ya kuikanyaga katiba kwa kupoka uhuru na haki hiyo ilipopiga marufuku mikutano ya kisiasa kwa vyama vya upinzani," anakumbusha Mbatia.

Aidha, anasema: "Katiba hii inatupa shida kwa sababu ya vipengele, ndiyo maana wanazuoni wataalamu wa katiba wanasema iwe ni mawazo, yanayotokana na umma tena ujiongoze."

### MADARAKA MAKUBWA

Suala jingine la kurejea upatikanaji wa katiba mpya, Mbatia anataja kuwa ni mamlaka makubwa aliyo nayo Rais. Mkuu wa nchi ana madaraka makubwa mno ikiwamo kuwateua viongozi mbalimbali kuanzia majaji, mabalozi, wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi.

Mbatia anasema mchakato wa upatikanaji katiba ulianza Juni 11 na 12, mwaka 1991 baada ya kukutana na wadau kadhaa kuweka msukumo wa kuandikwa nyingine mpya na kuanzishwa kwa vyama vingi vya siasa.

"Nasema wakati huo ilianzishwa kamati ya mabadiliko ya katiba mpya na rais wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, akaunda Tume ya Jaji Nyalali. Alitaka iulize Watanzania wanahitaji utaratibu gani, na ripoti ya Nyalali ikaja na mapendekezo mazuri, ingawa hayakutekelezwa mengi, lakini kwa kiasi kikubwa, lilibebwa wazo la kuanzishwa vyama vingi," anasema Mbatia.

Anautaja mtazamo wake kuwa ni kuundwa kwa tume ya mabadiliko ya katiba ambao itafanikisha kupatikana muafaka wa kufikia katiba mpya.

Mbatia anasema mwaka 1933 huko Uruguay, utaratibu wa kidunia uliwekwa kwamba ili nchi iitwe dola, inahitaji kuwa na tabia kuu nne.

"Watu, eneo la ardhi, mamlaka, mahusiano na nchi nyingine. Kuna tofauti kati ya dola na vyombo vinavyoisimamia dola, hapa kwetu inashindikana kufanyika ingawa mchakato ulianzishwa licha ya kuwapo uthubutu wa JK, changamoto inabakia kuwa Rais wa nchi hii bado ana mamlaka makubwa mno," anasema Mbatia.

INAENDELEA UK. 12



Lazaro Nyalandu,

# Nyalandu hakukosea kutoka, kurudi CCM

**Na John Kimbute**

KURUDI 'kundini' kwa Lazaro Nyalandu, aliyewahi kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii awamu ya nne na kiongozi wa kanda wa CHADEMA, ambacho ni mpinzani mkuu wa CCM ni tukio lililoleta shangwe katika mkutano mkuu maalum wa chama tawala jijini Dodoma.

Wiki iliyopita maamuzi ya Nyalandu, yaliamsha wengi vitini wakati wana- CCM walipokutana Dodoma kwenye Mkutano Mkuu wa chama kumchagua Rais Samia Suluhu Hassan kuwa mwenyekiti kujaza nafasi iliyoachwa wazi na hayati John Magufuli, aliyefariki Machi mwaka huu.

Alikuwa ni Mwenyekiti mpya wa chama, Rais Samia, aliyetambulisha ujio wake CCM kama 'zawadi' kwa wajumbe.

Hata hivyo kile alichosema Nyalandu kwa wajumbe ndicho ambacho kilikwenda mbali katika kuwashtua wana CCM hao, kuona taadhima ya suala hilo. Anautaja upweke wa kuwa katika upinzani, kuwa ziko 'nyimbo' ambazo unaimba ukiwa na furaha, ukihama huwezi kuziimba tena.

Ni rahisi kusema kuwa aliongeza chumvi lakini kwa hulka ya mantiki hakuna mtu anayeweza kusema uongo moja kwa moja, ila apindishe ukweli au atoe yaliyo katika hisia zake, hivyo unaweza kusema 'alitoa siri,' kuwa alijitahidi tu kwenda upinzani, mwishowe yakamshinda, hakuweza kuvumilia.

Ila kama ilivyokuwa kwa wale waliorudi CCM wakati wa awamu ya tano, kila anayerejea nyumbani anafanya hivyo kwa viwango tofauti kulingana na yeye alivyo, ukilinganisha na hali iliyopo.

Kwa maana hiyo wako ambao walirudi CCM kwa maana ya kuwa takriban wote wanaanzia Umoja wa Vijana, halafu 'wanasepa' kwa kuunga mkono wakati huo, juhudi za Rais John Magufuli na uzalendo wake katika kuwahudumia Watanzania.

Kusema kulikuwa na mwelekeo wa kizalendo ni njia mojawapo ya kuangalia kilichokuwapo, mtazamo ambao kimsingi una nguvu ya kiitikadi kuliko maelezo tofauti.

Hata hivyo, kulikuwa na upande wa pili ambao sasa umeondolewa. Kubanwa, kudhibiti shughuli za wazi za kisiasa na kwa maana hiyo mzunguko wa kawaida wa kupashana habari au kuzitafuta na kuzitoa kwa njia za kawaida za magazeti, redio na luninga.

Hali hii sasa imebadilika na pengine unaweza kwa dhati kusema kuwa Nyalandu amevutiwa na mabadiliko hayo, kuwa hana tena sababu ya kuwa upinzani kwa sababu hapingi kilichopo anakiri pia kuwa upinzani si lelemama.

> "Unaweza kuona ni tukio dogo la hisani kwa 'kijana' wa kisiasa ambaye sasa anaelekea umri wa miaka 50, kwa mtu mzima aliyeshafikia miaka 70 ya umri si kitambo sana.

Ukiangalia suala hilo kwa mwelekeo huo utamwelewa kikamilifu waziri huyo wa zamani, kwa maana ya usahihi wa kuondoa CCM na pia kurudi, siyo kwa sababu kila mmoja alitakiwa afanye hivyo ila kuelewa au kutambua ulazima kiasi chake wa kufanya hivyo kwa nyakati hizo tofauti.

Ni aina ya jitihada ya 'kuvaa viatu vyake' uangalie alivyoona hali halisi wakati ule na sasa, kuona mantiki ya kila hatua katika wakati wake, na siyo kujikanganya, kukosa msimamo au kutangatanga katika siasa.

Na kwa njia hiyo pia ameweza kuleta tukio, lililochangia uchangamfu kisiasa kwa wakati uliopo lijenge mshikamano.

Kwa mfano kuna jamii isiyo ndogo ya waliokuwa upinzani baada ya kufikia ngazi kubwa tu katika serikali na akitoa salamu zake, Nyalandu alimtaja mmojawapo aliyekuwa kwenye hadhara ile, Waziri Mkuu mstaafu Fredrick Sumaye, akitoa mfano wake kwa kusema 'baba yangu Sumaye.'

Unaweza kuona ni tukio dogo la hisani kwa 'kijana' wa kisiasa ambaye sasa anaelekea umri wa miaka 50, kwa mtu mzima aliyeshafikia miaka 70 ya umri si kitambo sana.

Ila kuna ngazi ya kisiasa ambayo Nyalandu aliwawezesha wengine kwa ushuhuda huo, wampatie waziri mkuu huyo mstaafu na kubadili mtazamo ili iwepo taadhima.

Ni jambo ambalo linaweza kuonekana kama lilianza kujengeka wakati wa hayati Magufuli na linaendelea hadi sasa huko nyuma ilikuwa nadra kiasi lakini wimbi la kuhamia CCM kutokana na siasa za kizalendo lilileta mabadiliko katika hisia za wengi. Imekuwa kana kwamba kuwapo katika chama ni kukubaliana kiasi tu na mwelekeo wake na kuhama kurudi CCM ni kutofautiana kiasi tu na upinzani au kutojisikia vyema.

Siyo kutangaza uadui na upinzani ila ni kutaka kuwa huru zaidi, hasa pale ambapo tunu za uongozi wa nchi ambazo kada husika anazithamini tayari zinafuatwa au zinaheshimiwa.

Ilikuwa ni sera za uzalendo kwa makada wengi tu wa CHADEMA ambao kwa jumla walikuwa vijana wa umri mdogo wenye 'damu inayochemka,' wakarudi au kuhamia CCM.

Mabadiliko ya sasa ya kurudisha misingi ya uhuru wa kukutana, kujieleza na utetezi wa demokrasia kwa jumla ni mabadiliko.

Inatosha kabisa kwa kiongozi kama Nyalandu, aweze kusimama mbele za watu bila 'hiana' au haya na kutangaza kuwa sasa anakubaliana na kinachoendelea katika uongozi, na hivyo anarudi nyumbani.

# Mbatia vs Awamu ya Sita

**INATOKA UK. 11**

**VYAMA VISIVYOSHINDANI**

Akizungumzia kuhusu kuwapo kwa vyama ambavyo havina ushindani kisiasa anasema kunatokana na katiba ambayo haitoi uhuru wa kidemokrasia kwa usawa na haki.

"Maendeleo ni watu, kurudishwa nyuma kwa vyama vya siasa katika uwanja huru wa kidemokrasia, kunatokana na kuitumia katiba hii hii. Dola limezuia mikutano na kampeni za kisiasa yote haya yanarudisha nyuma juhudi za kwenda mbele."

"Vyama vya siasa vimebaki kuzungumzia, udini, ukabila, kutokana na kukosa hoja imara za kisiasa, fikra zimerudi nyuma hakuna kufikiri shughuli za msingi katika kulijenga taifa," anaonya Mbatia na kuongeza kuwa kilichobakia ni kusema kwanini vyama havina hoja? Watazitoa wapi wakati wanabanwa.

Mbatia anaishauri serikali ya awamu ya sita inayosimamiwa na Rais Samia Suluhu Hassan, kutoa fursa ya upatikanaji wa katiba mpya ambayo itarekebisha masuala kadhaa ingawa hayawezi kumalizwa yote, kitakachobakia kitaendelea kushughulikiwa.

Kati ya masuala ambayo anasema yataleta mabadiliko kupitia katiba mpya ni haki na uhuru kamili kwa vyama vya siasa.

Mbatia anasema vyama hivyo vipo kwa ajili ya kushindanisha hoja ambazo hutoa mwongozo kwa serikali. "Utaratibu huu ili ufanyike kuna katiba iliyoweka misingi. Katiba ya sasa ya mwaka 1977, inatoa nafasi, haki ya chama cha siasa kufanya kazi kwa misingi iliyowekwa.

"Kuna kanuni, sheria, ili kujumuika pamoja, kufanya mikutano ya hadhara kwa vyama, ni haki ya kimsingi. Pamoja na mabadiliko yote yaliyofanyika katika katiba hii bado imebaki kuwa ya mfumo wa chama kimoja cha siasa, itikadi imeandikwa kwenye katiba kuwa ni ya ujamaa na kujitegemea.

"Ibara ya 10 ilikuwa inasema CCM itakuwa ni chama pekee ilifutwa. Ilivyofutwa na nyingine zikabaki kama zilivyo, hii inatupa shida, japo ibara moja inatoa haki, nyingine inafinyanga haki hiyo na kuendelea kuturudisha nyuma."

## JAMILA BORAFYA:

# Wawakilishi sikilizeni jambo linalokwaza wenye ulemavu

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

"KATI ya wawakilishi 50 wa majimbo ya uchaguzi ya Zanzibar waliomo katika Baraza la Wawakilishi (BWW), hakuna mwenye ulemavu kutoka jimboni licha ya watu wanaoishi na ulemavu kujitokeza kugombea nafasi hiyo katika uchaguzi mkuu uliopita."

Ni madai ya Jamila Borafya Hamza, aliyekuwa miongoni mwa waliojitokeza kugombea uwakilishi katika Jimbo la Mwanakwerekwe kiswani Zanzibar, anapozungumza na Nipashe.

Licha ya kwamba Jamila au Chocolate Colour, wajumbe hawakumpa nafasi, mwanamama huyo aliyetaka kuvunja ukimya na kuonyesha nguvu waliyo nayo wenye ulemavu anasema hajakata tamaa.

Anakumbusha kuwa maishani Waswahili wanasema, ni dhambi kukata tamaa kwa sababu hujui wapi mafanikio yako yataanzia, licha ya kwamba unapitia kwenye lindi la changamoto.

Anaamini kuwa wanashauri kutokukata tamaa kwa sababu ni ishara ya kushindwa kwa sababu wapo waliofanikiwa baada ya kupiga moyo konde na kukabiliana na shida na dhiki nyingi na hatimaye kushinda.

Jamila anayeishi na ulemavu wa uoni, akiwa na miaka 23 ni mfano wa wasichana wenye mahitaji maalumu waliojitokeza na kujitosa kugombea nafasi ya uwakilishi Jimbo la Mwanakwerekwe katika uchaguzi mkuu wa 2020.

Jamila licha ya ulemavu alionao hakukata tamaa kugombea nafasi hiyo kutokana na vikwazo mbalimbali alivyokumbana navyo wakati akijiandaa kupanda jukwaani ikiwamo kukatishwa tamaa na baadhi ya wananchi.

Anasema wakati wa mchakato wa kugombea nafasi hiyo, aliingia ulingoni na alikuwa mwanamke pekee mwenye ulemavu aliyejitokeza kati ya wanachama 12 wa CCM.

Anaeleza kuwa wapo waliomkatisha tamaa kutokana na ulemavu huo na wengine waliomshauri aende akagombee nafasi ya viti maalum na kuachana na uwakilishi jimboni.

"Niligoma kugombea viti maalum niliwaambia hata kama nitashindwa katika mchakato wa kura za maoni lengo langu ni kujiingiza kwenye uwakilishi kwa sababu uwezo wangu ni kulitumikia jimbo na siyo viti maalum kama wanavyonishauri," anasema.

Ndoto zake ni kuwa mwanasiasa anayewakilisha jimbo kwa sababu, wanawake wengi wanaogopa kwenda majimboni ndiyo maana wengi wao wanang'ang'ania viti maalum na wenye mahitaji wanaingia barazani kupitia viti vya walemavu, lakini hakutaka kubebwa ila kujiwezesha mwenyewe.



Jamila anatamani kuwa mwakilishi akianzia mapambano jimboni. **PICHA: RAHMA SULEIMAN.**

Jamila anaongeza: "Safari yangu ya kuwa mwakilishi wa Mwanakwerekwe iliishia katika mchakato wa kura za maoni na kukatisha ndoto zangu...wajumbe walifanya ujumbe wao na sikubahatika kupata hata kura moja," anasema.

Katika mchakato huo alijifunza mambo mengi ikiwamo kujiamini kwa sababu uwezo anao na bado hajakata tamaa na kusema kuwa ipo siku umuhimu wake utaonekana.

Anaamini miongoni mwa sababu zilizomwangusha kutochaguliwa ni ulemavu anaoishi nao na kutokuwa na zawadi kwa ajili ya kuwapatia wajumbe ambao inabidi ujue 'unawaachaje'.

> Wakati wa kuomba kura niliwaambia wajumbe kinachokwenda kuwatumikia katika Baraza la Wawakilishi si macho yangu wala ulemavu...

"Wakati wa kuomba kura niliwaambia wajumbe kinachokwenda kuwatumikia katika Baraza la Wawakilishi si macho yangu wala ulemavu nilionao bali ni akili na maarifa na kuziwasilisha changamoto za wananchi," anasema.

Anaongeza kuwa fedha ni kikwazo kwa wanawake kugombea katika nafasi za uongozi kwa sababu uchaguzi ni gharama, hivyo wengi wenye kipato cha chini wanashindwa kugombea nafasi za uongozi licha ya kwamba wanawake wanaweza.

Jamila anaanza harakati za kugombea nafasi za uongozi tokea akiwa shule za msingi ambapo aliwahi kuwa Waziri wa Habari wa Serikali ya Wanafunzi Shule ya Kisiwandui.

Aidha, anasema mwaka 2016 alishiriki katika Bunge la Vijana na Mwenyekiti wa Baraza la Vijana wa Shehia ya Mwanakwerekwe na kwamba kukosekana nafasi ya uwakilishi wa Jimbo la Mwanakwerekwe, hakujadidimiza ndoto zake za kuwa kiongozi hivyo ataendelea kupambana na kumfikisha anapopataka ili kutimiza azma yake ya kuwa mwakilishi.

**USHAURI**

Jamila anashauri ili wanawake washike nafasi nyingi za uongozi nilazima kwanza jamii iwaamini hasa wenye ulemavu. Ifahamu kuwa wana uwezo na mchango mkubwa kwa sababu wanaweza kujitolea, kupambana na kuleta mafanikio.

Aidha, anataka serikali kurekebisha sheria ambazo zitawapa fursa wanawake hasa majimboni, vyama vya siasa kuweka vipengele maalum vinavyowapa nafasi wanawake na watu wenye ulemavu.

"Kwa mfano katika Baraza la Vijana sheria namba 16 ya mwaka 2013 inaweka wazi kwamba katika uchaguzi wowote kama kutakua na mtu mwenye ulemavu au mwanamke akigombea apewe kipaumbele," anasema.

Anawataka wanawake waliopata nafasi za uongozi wasiwaangushe wanawake wenzao kwa sababu watakapofanya vibaya wengine watakuwa hawaaminiki katika jamii lakini watakapofanya vizuri watawaonyesha njia nzuri kwa kufikia katika nafasi za uongozi.

Anawashauri wanawake wajitokeze wagombee nafasi za uongozi na wasikate tamaa kutokana na changamoto mbalimbali na wapambane ili kuwa na wanawake wengi katika vyombo vya maamuzi.

**CHANZO CHA ULEMAVU**

Jamila anasema alizaliwa na ulemavu wa macho na sababu ya kuupata anaelezwa kuwa ni homa kali aliyopata mama yake wakati alipokuwa mjamzito na kwamba tatizo liliongezeka baada ya kutumiwa dawa ili kuitibu lakini bahati mbaya ilimwathiri mtoto na kumsababishia upofu.

Mwanasiasa huyo amemaliza kidato cha nne mwaka 2019 katika Shule ya Sekondari ya Haile Selasie, mjini Unguja lakini alishindwa kuendelea na masomo kutokana na matatizo ya afya na kwa mujibu wa ripoti kutoka kwa daktari wake kuwa ana tatizo jingine linalomsumbua kwenye mfumo wa damu.

Anaamini kuwa atakapopata matibabu na afya yake itakapoimarika ataendelea na masomo na lengo lake ni kusomea masuala ya elimu ya usimamizi na uongozi ili kutimiza ndoto zake.

# THOMAS SANKARA, PAT LUMUMBA: MASHUJAA 'WALIOCHINJWA' KITATANISHI

Na Joseph Mwendapole


HISTORIA ya uongozi wa Afrika kwa kiasi kikubwa umejengwa kwenye mapinduzi yaliyosababisha viongozi waliokuwa madarakani kupinduliwa hata kuuawa na washirika wao wa karibu kama ilivyotokea kwa Thomas Sankara na Patrice Lumumba.

Rais Thomas Sankara ambaye ni rais wa zamani wa Burkina Faso aliyeingia madarakani kwa mapinduzi mwaka 1983 aliuawa na mshirika wake wa karibu akishirikiana na kikundi cha wanajeshi lakini mazingira halisi ya mauaji yake hayajafahamika.

Uchunguzi wa mwili wake uligundua kwamba alikuwa umechanwa kwa kupigwa risasi nyingi, wakili wa familia yake alisema.



Patrice Lumumba



Thomas Sankara

**UTATA KIFO CHAKE:**

Ukweli haujabainika kuhusu mazingira na wale waliohusika wakati wa mapinduzi ya utawala wake mwaka wa 1987.

Mjane wake Mariam Sankara, anatafuta haki na vipimo vya vinasaba (DNA) vilivyofanywa kwenye mabaki yanayodaiwa kuwa ya kiongozi huyo, lakini havikuwa kamilifu.

Kufuatia kifo chake, waranti wa kimataifa wa kukamatwa aliyekuwa rais wa nchi hiyo Blaise Compaoré, anayeishi uhamishoni na ambaye alikuwa Rais wa Burkina Faso mwaka 1987 hadi 2014, uliotolewa.

Jenerali Gilbert Diendere, ambaye baada ya kifo cha Sankara alikuwa mkuu wa ujasusi wa Compaore, alikuwa karibu sana na Sankara wakati wa mauaji yake.

Inaripotiwa kuwa Sankara alishirikiana kwa karibu na mashirika ya ujasusi ya Marekani na Ufaransa na kufanikisha kuachiliwa mateka wa mataifa ya magharibi waliokuwa wakishikiliwa mara kwa mara na makundi ya kijihadi huko Afrika Magharibi.

**UCHUNGUZI WA KARIBUNI**

Hivi karibuni jopo la majaji wa mahakama ya kijeshi lilimtaja rais wa zamani Burkina Faso Blaise Compaoré, anastahili kushtakiwa kwa mauaji ya Sankara, aliyempindua mwaka 1987.

Hali hiyo kwa walio wengi wanaona imefungua matumaini ya uwezekano wa kupatikana kwa haki kuhusu mauaji yake.

Compaoré alikimbia mafichoni Ufaransa 2014 baada ya kushindwa katika jaribio la kutaka kubadilisha sheria ili kuendeleza muda wake madarakani na waranti ya kukamatwa kwake ilitolewa 2015.

Mahakama hiyo ya kijeshi mwezi uliopita ilisema Compaoré anastahili kushtakiwa kwa 'kushambulia taasisi za usalama wa taifa na kuhusika na njama ya mauaji ya Sankara na kuuficha mwili wake.

Uwezekano wa kushtakiwa kwa Compaoré, kwa mauaji hayo huenda ukamaliza jitihada za muda mrefu za wafuasi wake kutaka kupata haki.

Sankara, anayeitwa 'Che Guevara wa Afrika' alipendwa sana katika nchi yake na barani Afrika. Uamuzi huo wa korti ya kijeshi utarejesha tena katika mijadala mauaji ya Sankara na kiongozi mwingine pendwa wa Patrice Lumumba, aliyekuwa na umaarufu kama wake wakati wa miaka ya 1960 akiiongoza DR Congo.

Je, ni nani aliyehusika na mauaji ya viongozi hao wawili ambao wanatajwa kuwa mashujaa wa bara hili? Ni kitandawili.

Thomas Sankara shujaa kwa vijana wengi wa Kiafrika katika miaka ya 1980 amebaki katika kumbukumbu za wengi tangu alipouawa akiwa na miaka 37.

Wengi hadi sasa wanamuenzi Sankara kwa njia mbalimbali akiwamo mwanasiasa wa Afrika kusini Julius Malema kuvaa kofia yake nyekundu ya kijeshi iliyotambulika kama sehemu ya vazi la Sankara.

Alisifiwa na wafuasi wake kwa uadilifu kuwa kiongozi asiye na ubinafsi, nahodha wa jeshi na mwanamapinduzi anayepinga ubeberu akiongoza Burkina Faso kwa miaka minne kutoka 1983-87.

Ingawa Sankara anaweza kuwa lebo ya mapinduzi, kama Che Guevara mzaliwa wa Argentina, teksi nyingi kote Afrika Magharibi zina stika ya picha yake kwenye vioo vya magari.

**ANAVYOKUMBUKWA**

Anakumbukwa kwa kujaribu kuibadilisha nchi yake ya Afrika Magharibi kuwa maabara ya kilimo ili kujitosheleza kwa chakula.

Wakati wa enzi yake, alipigia debe bidhaa zilizotengenezwa nchini Burkina Faso na kuimarisha uzalishaji na utumiaji wake.

Rais huyo wa Burkina alitaka kuimarisha mfumo wa afya na elimu katika nchi ambayo ilikuwa moja ya mataifa maskini zaidi duniani. Alikuwa na maisha ya wastani yeye mwenyewe. Uhuru wa wanawake pia ulikuwa mojawapo ya mambo aliyoyapa kipaumbele.

Karibu miongo mitatu baada ya mauaji yake, anaonekana kuwa shujaa na watu ambao waliuangusha utawala wa Blaise Compaoré mnamo Oktoba 2014.

Wengi wanamtambua kuwa shujaa wa vijana wa Afrika na mradi wa kuweka kumbukumbu yake unaendelea jijini Ouagadougou nchini humo.

**KUKOSOLEWA**

Uhusiano wake na kiongozi wa Libya Kanali Muamar Gaddafi, lakini kwa kuvuruga utaratibu na mifumo iliyowekwa. Mwaka 1985, mgogoro ulizuka na Mali kuhusu mpaka kati ya nchi hizo mbili.

**PATRICE LUMUMBA DRC**

Huyu ni Waziri Mkuu wa kwanza wa Congo aliyechaguliwa mwaka 1960 na kuondolewa madarakani muda mfupi kama ilivyokuwa kwa Sankara.

Kulikuwa na uasi wa jeshi wakati vikundi vya wanajeshi vikijitenga kutoka mkoa wenye utajiri wa madini wa Katanga wakifanya harakati zao na wanajeshi wa Ubelgiji ambao walirudi wakidai kuwa walikuwa wamekuja kurejesha usalama Congo.

Lumumba alichukua hatua kwa kuugeukia Umoja wa Kisovyeti kwa msaada hali iliyosababisha hofu Uingereza na Marekani ambao waliogopa Wasovieti watapata nafasi katika Afrika kama vile walivyofanya nchini Cuba.

Katika Ikulu ya White House, Rais wa Marekani wakati huo Dwight D. Eisenhower, alifanya mkutano wa Baraza la Usalama la Kitaifa mwaka 1960 na alimgeukia Mkurugenzi wa Shirika la Ujasusi la Marekani (CIA) na kutumia neno "kuondolewa" kwa kile alichotaka kifanyike kwa Lumumba.

CIA ilianza kufanya kazi na kuandaa mipango kadhaa pamoja na kikosi maalum na dawa ya meno yenye sumu ili kumua kiongozi huyo wa Congo ingawa hayakufanyika kwa sababu wakala wa CIA aliyekuwa Congo , Larry Devlin, alikataa akisema anasita kuitekeleza mipango hiyo.

Pamoja na kukataa huko, Januari 1961, Lumumba, alikuwa amefariki swali likabaki je, Uingereza na Marekani zilihusika na mauaji yake?

Mauaji yake yanadaiwa kutekelezwa na wapiganaji kutoka Congo pamoja na Wabelgiji na kwa kusaidiana na serikali yao ambayo ilimchukia sana.

Hadi leo mauaji ya Lumumba yamegubikwa na taarifa nyingi na ukweli wa kilichotokea huenda hautajulikana hivi karibuni.

**BBC**



# Waitara avalia njuga mil. 26/- mabasi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema itafuatilia zaidi ya Sh. milioni 26 za wadau wa usafirishaji wa mabasi, ambazo zimepotea kutokana na kutumia mfumo wa mashine za kielektroniki unaotumika kukata tiketi za abiria wa mikoani.

Aidha, wadau wa usafirishaji wameiomba serikali kumwondoa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) kutokana na kukerwa na mwenendo wa uendeshaji wa mamlaka hiyo, ikiwamo kuwatumia wao kama sehemu ya kuvuna fedha na si kujali kero wanazokabiliana nazo.

Akizungumza katika mkutano na wadau wa usafirishaji, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, alisema fedha hizo haziko serikalini wala kwa wamiliki wa kampuni za wafanyabiashara wa mabasi ambayo yanafanya safari katika mikoa mbalimbali nchini.

Waitara alisema kutokana na yeye kupokea malalamiko kutoka kwa wadau tofauti ambao wanalalamikia mfumo huo wa ukatishaji tiketi kwa kutumia mashine za kielektroniki, ameamua kuitisha kikao hicho ili kuwasikiliza na kufanyia kazi suala hilo.

"Nimesikia hizi changamoto (kero) zenu ikiwamo fedha mnazoweka katika mashine za POS (za kielektroniki) ambazo zinatumika kukatisha tiketi za abiria ambazo baadaye zinatakiwa kurejeshwa kwenu lakini hamzipati kwa wakati," alisema Waitara.

Aliwataka wafanyabiashara hao wawe na imani na serikali ndiyo maana amewaita ili waseme kile kinachowatatiza kutokana na kutumia mfumo wa ukatishaji tiketi kimtandao (e-ticketing).

Hata hivyo, alisema alishazungumza na Mkurugenzi Mkuu wa LATRA kuhusiana na kero ambazo wanakutana nazo wadau wa usafirishaji ikiwamo faini wanazolipishwa na LATRA.

"Nyie ni watu muhimu sana katika serikali hii. Niwewasikiliza ni lazima tuondoe changamoto (kero) katika sekta hii ili mradi mmesema vizuri kwamba hakuna mtu ambaye anataka kukwepa kulipa kodi, watu wote mlipe kodi," alisema Waitara.

Naye mdau wa usafirishaji Rogers Tupondige, alisema serikali inapaswa kuingilia kati suala hilo kutokana na kwamba LATRA iko kwa ajili ya kuwakandamiza na si kuwasaidia kama inavyoeleza.



Mchuuzi wa vikapu akisubiri wanunuzi katika soko la stendi ya Sabasaba, jijini Dodoma jana. Kikapu kimoja kiliuzwa kwa bei ya 3,000/-. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Miradi minne kuipatia Dodoma umeme

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema inatekeleza miradi minne ya umeme katika mkoa wa Dodoma ili kuhakikisha maeneo yote yanapata huduma hiyo na kuwawezesha

wananchi kufanya shughuli za kiuchumi.

Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alisema hayo wakati akiwasha umeme katika kijiji cha Makutupa kilichoko wilayani Kongwa mkoani hapa.

Dk. Kalemani aliitaja miradi inayotekelezwa kuwa ni wa kusambaza umeme vijijini, unaoendelea sasa wa awamu ya tatu ambao mzunguko wa

kwanza unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi mitatu.

Pia alisema miradi mingine ni ya kupeleka umeme vitongojini, mradi wa kupeleka umeme kwenye maeneo yaliyo karibu na mitaa mijini na miradi inayotekelezwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Alisema endapo miradi hiyo itakamilika yote kwa wakati itaviwezesha vijiji mbalimbali kupata nishati ya umeme hali itakayoamsha wakazi wa maeneo hayo kuendesha shughuli za kiuchumi katika maeneo mbalimbali.

"Serikali imetoa Sh. bilioni 60 katika mradi wa kusambaza umeme vijijini mkoani Dodoma wa kupeleka umeme vitongojini. Imetoa Sh. bilioni 48.3, kwa mradi wa Peri-Urban imetoa shilingi bilioni 23 na ule unaotekelezwa na fedha kutoka TANESCO kama ilivyo hapa Makutupa," alisema Dk. Kalemani.

Kalemani alisema katika kazi ya usambazaji umeme katika vijiji mbalimbali mkoani Dodoma, takribani vijiji 467 kati ya 581 vimeshasambaziwa nishati hiyo ambayo ni zaidi ya asilimia 81 na kwa vijiji vilivyobaki kazi inaendelea.

Hata hivyo, waziri huyo amebainisha kuwa katika wilaya ya Kongwa ni vijiji vinne tu ambavyo havijafikiwa na umeme kati ya vijiji 87.

Pia Kalemani alitembelea eneo la Mbande ambalo wananchi wake wamekuwa wakilalamika kuwa kuna nguzo za umeme zilizosimikwa muda mrefu bila wananchi kuunganishiwa umeme.

Akiwa katika eneo hilo, Dk. Kalemani aliwaahidi kuwa mkandarasi, kampuni ya Derm Electric, ataanza kuwaunganishia umeme wananchi kuanzia Mei 7, mwaka huu.

Hata hivyo, aliwasisitiza wananchi kutumia umeme kwa matumizi mbalimbali kwa kuwa serikali inatumia fedha nyingi kufikisha huduma hiyo katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo kupunguza gharama za uunganishaji ili

kila Mtanzania atumie nishati hiyo.

Kadhalika, Dk. Kalemani amepiga marufuku kwa wananchi kununua nguzo za umeme ili waunganishiwe umeme huku akiweka msisitizo wa gharama za

kuunganishiwa umeme kuwa ni Sh. 27,000.

Alisema vijiji 1,974 kati ya 12,268 ambavyo bado havijasambaziwa umeme kwa nchi nzima, makandarasi wa kusambaza umeme kwenye vijiji hivyo

wameshapatikana na wataingia katika maeneo ya kazi wiki ijayo.

Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Dk. Suleiman Serera, alimshukuru waziri na wizara yake kwa kazi ambayo wamekuwa wakiifanya ya kusambazia

wananchi huduma ya umeme ambayo inazidi kuimarisha uchumi wao.

"Kama unavyojua katika eneo letu la Dodoma linahitaji sana umeme na wilaya yetu ya Kongwa shughuli nyingi zimefanyika tunavyo vijiji 87 tunaishukuru sana wizara yako, vijiji 79 umeme umefika," alisema Dk. Serers.

## Machinga waonywa uvamizi wa maeneo

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAFANYABIASHARA wadogo katika soko la Sabasaba jijini Dodoma, wameonywa kutovamia maeneo yaliyo wazi ambayo yanamilikiwa kisheria na halmashauri ya jiji.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana na Mwenyekiti wa Soko hilo, Athumani Makole, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kufafanua kuhusu ubomoaji wa vibanda vipya vilivyojengwa na wamachinga kwenye eneo la hifadhi ya jiji.

Makole alisema vibanda hivyo vinaondolewa kutokana na kujengwa bila kushirikishwa uongozi uliopo unaotambuliwa na ofisi mbalimbali ikiwamo ya mkuu wa mkoa.

Alisema kutokana na ukiukaji huo ambao haukufutwa sheria za kuruhusu kujenga maeneo hayo yaliyobomolewa ni wazi kuwa machinga wamevunja sheria, hivyo wanatakiwa kuepukana kuvamia sehemu zilizotengwa.

"Kuna maeneo mbalimbali yamezuiwa ikiwamo humu ndani ya soko hili la Sabasaba. Jiji limezuia kufanya biashara wala kujenga vibanda. Sasa hao ndugu zangu wameenda kujenga kwenye maeneo hayo bila kuwa na kibali chochote wala cha kuuomba uongozi wa soko, hivyo wanastahili kubomolewa kama sheria inavyokataza," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema machinga wanatakiwa kufuata sheria na kanuni pindi wanapohitaji maeneo ambayo wanataka kufanya biashara ili kuepukana na hasara wanazozipata kwa kuharibiwa mali zao.

Baadhi ya machinga waliovunjiwa vibanda hivyo, waliwaambia waandishi wa habari kuwa wamejenga bila kufuata utaratibu kutokana na wengi wao kukosa maeneo.

Onesmo Timotheo, mmoja wa machinga hao, alisema hivi sasa watahakikisha wanafuata sheria na kanuni ili kupatiwa maeneo ambayo watakayofanya biashara bila kubughudhiwa.





# Watishia kuandamana kisa kina Mdee

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

LICHA ya Spika wa Bunge, Job Ndugai, kufafanua uhalali wa wabunge 19 wa Viti Maalum wanaotokana na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Baraza la Wanawake la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA) Mkoa wa Mbeya limetishia kuhamasisha maandamano ya wanawake nchi nzima kushinikiza Bunge kuwaondoa bungeni wabunge hao.

Baraza hilo limedai kuwa uwapo wa wabunge hao ndani ya chombo hicho cha kutunga sheria ni kinyume cha Katiba ya nchi.

Wakizungumza kwenye mkutano wa BAWACHA uliofanyika juzi jijini hapa, wajumbe wa baraza hilo walisema chama tayari kimeshawatimua wabunge hao kwa mujibu wa katiba, hivyo kitendo cha Spika Ndugai kuendelea kuwakumbatia ni kuvunja Katiba ya nchi inayoelekeza kila mbunge lazima atokane na chama cha siasa.

Akitoa tamko baada ya kumalizika kwa kikao hicho, Mwenyekiti wa BAWACHA Mkoa wa Mbeya, Elizabeth Mwakimomo, alisema hawatavumilia kuona Katiba ya nchi ikivunjwa na badala yake watahamasisha maandamano ya wanawake nchi nzima kupinga uvunjifu huo wa katiba.

"Sisi BAWACHA Mkoa wa Mbeya, tunasisitiza kuwa wale si wabunge halali kwa kuwa hawana chama chochote cha siasa. Hii ni kwa sababu kwenye chama chetu wameshafukuzwa, hivyo hatutavumilia kuona Spika akiendelea kuvunja katiba na sisi tumenyamaza. Endapo hatawaondoa, tutaandamana nchi nzima mpaka Dodoma kuhakikisha wabunge hao wanaondolewa," alisema Mwakimomo.

Aliongeza kuwa kitendo cha Spika Ndugai kuhoji uhalali wa wabunge hao kutimuliwa ndani ya chama, si jukumu lake kwa vile sheria inawataka kuwasilisha barua ya kutimuliwa kwao bungeni jambo ambalo CHADEMA ilishalitekeleza.

"Sheria haituelekezi tupeleke muhtasari wa kikao ili aione Ndugai bali inatutaka kupeleka barua ya kuonyesha kuwa wanachama hao tumeshawafukuza. Hilo tumeshalitekeleza na si jukumu la Ndugai kujua kama tumewafukuza kwa namna gani. Hilo ni la wabunge wenyewe kwenda mahakamani kupinga kutimuliwa na si vinginevyo," alisema.

Mmoja wa wajumbe wa baraza hilo, Jesca Msoja alisema wabunge hao walichokifanya ni usaliti kwa chama chao ambao hauwezi kuvumilika, hivyo hawatakubali kuona wakiendelea kukaa bungeni wakila posho kwa kutumia jina la chama chao.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, Tabibu Lubandamo (katikati), akizungumza katika kikao cha Baraza la Madiwani, juzi. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Reuben Mfune na Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Daniel Kamwela. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Polisi wanasa mtandao wizi wa pikipiki

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, limenasa mtandao wa wizi wa pikipiki za matairi matatu, maarufu kama Bajaji, zinazoibiwa mkoani hapa na maeneo ya jirani.

Pikipiki hizo zinadaiwa kuwa baada ya kuibwa huuza nchi jirani ya Malawi kupitia mpaka wa Kasumulu wilayani Kyela.

Hatua hiyo ni baada ya dereva mmoja wa Bajaji kuokotwa katika eneo la Inyala nje kidogo ya Jiji la Mbeya akiwa hajitambui baada ya kudaiwa kukodiwa na watu asiowafahamu na kisha kuporwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema jana kuwa taarifa za kupatikana kwa mtu huyo zilitolewa na wasamaria wakidai yuko hoi hajitambui, hivyo wanahitaji msaada wa haraka.

Baada ya kupata taarifa hiyo, Kamanda Matei alisema walifika eneo la Inyala na kumkuta Ramadhan Rashid ambaye ni dereva Bajaji akiwa hoi hajitambui na kisha kufanya utaratibu wa kupata huduma za matibabu.

"Kumeibuka mtandao wa wizi ambapo kundi na watu hukodi Bajaji na kujifanya abiria kumbe wana lengo la kuteka abiria na kisha kutokomea na Bajaji ambazo huzisafirisha nje ya nchi ikiwamo Malawi kuziuza. Tayari tumeshapata taarifa za baadhi ya watu wanaojihusisha na tunaendelea na upelelezi baada ya kukamilika watakamatwa," alisema Matei. Rashid alisema alikodiwa na watu wasiojulikana na kisha kupewa chips ambazo zilimsababishia usingizi na baadaye kujikuta kwenye kituo cha polisi.

Alisema watu hao walijifanya wageni na wanahitaji kupelekwa eneo la Inyala na walikuwa radhi kutoa kiasi chochote cha fedha ili wafike na kwamba wakati wakiwa njiani alipewa chips na abiria hao na bila kujali alikubali.

Kwa mujibu wa Rashid, baada ya muda alianza kujisikia vibaya na kupoteza fahamu hadi alipojikuta yuko kituo cha polisi.

Alisema ni mara ya kwanza kukumbwa na kadhia hiyo na kwamba kuanzia sasa atakuwa makini kupakia abiria hasa nyakati za kuanzia jioni.

# DC awapigia debe waandishi wa habari

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, amewahamasisha waandishi wa habari kujiunga kwenye vikundi ili wapate mkopo wa asilimia 10 unaotolewa na halmashauri ambao utawasaidia kufungua miradi mbalimbali ya maendeleo na kuinua uchumi.

Ntinika alitoa rai hiyo juzi kwenye maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani ambayo pia yaliadhimishwa maeneo mbalimbali nchini.

Alisema wanahabari wanazungukwa na fursa mbalimbali lakini wanashindwa kuzitumia badala yake wamegeuka kuwa wasemaji wa watu wengine huku wao wakiendelea kutaabika.

Ni wakati sasa, alisema wa kuzitumia fursa zilizoko kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo mkoani Mbeya ambako kuna mikopo ya halmashauri, kilimo, biashara na uwekezaji mwingine ambao utawasaidia kujikwamua kiuchumi.

"Mnaposherehekea Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani tafakarini pia maisha yenu ya kihabari. Kila kazi lazima iwe na manufaa. Mna fursa ya kuonana na mtu yeyote, hivyo tumieni nafasi yenu kuongea na wadau wawapatie fursa na sisi serikali tuko tayari kuwaunga mkono," alisema Ntinika.

Aidha, alikiahidi Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Mbeya (MBPC) kuwapatia kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya chama hicho kwa gharama nafuu.

Mwenyekiti wa MBPC, Festo Sikagonamo, alisema wanahabari ni kiunganishi kikuu baina ya wananchi na serikali, hivyo wanahitaji kuthaminiwa kwa kuhakikisha heshima yao inalindwa ili kutimiza majukumu yao bila kikwazo.

Siku ya uhuru wa vyombo vya habari ni fursa kwa wanataaluma kujitathmini kujua walikotoka, walipo na wanakotarajia kufika sambamba na kushughulikia vikwazo vinavyowakabili.

Miongoni mwa waandishi wakongwe nchini, Ulimboka Mwakilili, aliwapongeza wahabari kwa kuendelea kuungana na kuwa wamoja katika nyakati mbalimbali wanazopitia.

Aliwasihi wanahabari kushirikiana kutimiza majukumu yao kwa kuhakikisha wanakuwa wamoja pindi wanapopata matatizo sambamba na kuendelea kuwahudumia Watanzania kwa kuwapatia habari zinazochochea maendeleo na uwajibikaji.





Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Dk. Saada Mkuya Salum (kushoto), akikabidhi cheti cha shukurani kwa utumishi uliotukuka kwa aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya kitaifa ya kuratibu na udhibiti wa dawa za kulevya, SACP Kheriyangu Mgeni Khamis, baada ya kumaliza muda wake wa utumishi kwa nafasi hiyo, katika hafla iliyofanyika wizarani Migombani, Mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waziri Mazrui ataka kinga ya maradhi kabla ya matibabu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, amewataka wananchi kujikinga na magonjwa mbalimbali ili kuepukana na gharama za kutafuta tiba wanapougua.

Aliyasema hayo katika hafla ya makabidhiano ya gari la kubebea wagonjwa na vifaa tiba lililotolewa na viongozi wa Jimbo la Mpendae kwa ajili ya kituo cha afya cha Mpendae Mjini Zanzibar.

Alisema wakijikinga na maradhi kutaepusha msongamano wa watu katika vituo vya afya, huku akisisitiza wananchi kutumia maji yenye viwango ili kuepukana na magonjwa ya mlipuko.

"Ukiweza kujikinga na maradhi gharama zinakuwa ndogo kuliko tiba ambayo inagharama kubwa," alisema.

Aidha, aliwapongeza viongozi wa jimbo hilo kutatua kikwazo cha upatikanaji wa majisafi na salama kwa sababu unatumia majisafi unajilinda na maradhi mbalimbali yakiwamo ya mlipuko.

Aliwataka wakazi wa jimbo hilo kushirikiana na viongozi bila kujali itikadi zao za kisiasa ili kupata maendeleo.

Naye Mbunge wa Jimbo la Mpendae, Taufiq Salum Turky, alisema gari hilo alilolitoa litasaidia kuharakisha wagonjwa hasa wajawazito ambao wana mahitaji ya dharura ya kupelekwa Hospitali ya Mnazimmoja.

Alisema atahakikisha wanaboresha huduma mbalimbali zikiwamo za afya, elimu, maji na miundombinu ya barabara za ndani ili kuondoa vikwazo vinavyowakabili wananchi. Alisema watawaletea maendeleo wananchi wa jimbo hilo bila ya kujali itikadi za vyama vya siasa, dini au tofauti zozote zile, huku akiwataka wananchi kushirikiana na serikali ili maendeleo yamguse kila mtu.

Mwakilishi wa jimbo hilo, Shabani Ali Othman, alisema vifaa walivyotoa ni miongoni mwa utekelezaji wa ahadi walizowaahidi wananchi wa jimbo hilo wakati wakiomba ridhaa ya kuliongoza jimbo.

Daktari wa kituo hicho cha afya, Hamad Khamis Ali, alisema wamepata faraja kupata gari hilo na vifaa tiba kwa sababu kituo hicho kinapokea wagonjwa wengi.

Alisema kikwazo kikubwa kipo katika huduma za wajawazito hususan wanapotaka kuwasafirisha ambao wanahitaji huduma za dharura kuwapeleka Hospitali ya Mnazimmoja.

## Baraza la Wawakilishi kuanza leo

**Na Mwandishi Wetu**

MKUTANO wa Tatu wa Baraza la Kumi la Wawakilishi Zanzibar unatarajiwa kuanza leo, ambapo maswali ya msingi 218 yanatarajiwa kuulizwa na kujibiwa katika mkutano huo.

Katibu wa Baraza hilo, Raya Issa Msellem, alisema katika mkutano huo pia kutakuwa na kiapo cha Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka Jimbo la Pandani kisiwani Pemba baada ya kushinda katika uchaguzi mdogo uliofanyika Machi mwaka huu.

Aidha, alisema kutakuwa na majadiliano ya bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2021/2022, na pia itawasilishwa miswada ya sheria na kujadiliwa katika mkutano huo.

Akiitaja miswada hiyo ni miswaada ya sheria ya fedha na muswada wa sheria ya kuidhinisha matumizi ya serikali kwa mwaka 2021/2022 pamoja na miswada ya kusoma kwa mara ya kwanza.

Alisema Baraza la Wawakilishi litaendelea kufanya kazi kwa karibu na vyombo vya habari ili kuhakikisha taarifa ambazo jamii zinapaswa kuwafikia zinawafikia kwa wakati.

**Aidha, alisema kutakuwa na majadiliano ya bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2021/2022, na pia itawasilishwa miswada ya sheria na kujadiliwa katika mkutano huo.**

# Sababu mafanikio udhibiti wa dawa za kulevya hizi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Mkuya Salum, amesema heshima, nidhamu na uzoefu umesababisha tume ya kitaifa ya kuratibu na udhibiti wa dawa za kulevya kutekeleza majukumu yake na kuleta mabadiliko makubwa kwa watendaji na jamii inayoitumikia.

Aliyasema hayo jana wakati wa hafla ya kumuaga aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa tume hiyo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Polisi, Kheriyangu Mgeni Khamis.

Dk. Saada alisema ujasiri na kujiamini kwake kumesababisha hata watendaji wa tume kuonekana wapo tayari muda wote kwenye kutekeleza majukumu yao na kufikia malengo kwa mujibu wa majukumu yao ya kazi katika kudhibiti dawa za kulevya na kuiletea heshima.

Aidha, Dk. Saada alimshukuru aliyekuwa mkurugenzi huyo kwa utumishi wake na namna alivyoweza kuisimamia taasisi yake pamoja na kuwashughulikia vyema vijana walioachana na matumizi ya dawa za kulevya kuona wanapata nafuu.

"Kumtoa mtu katika mazingira hatarishi ya matumizi ya dawa za kulevya na ukamtengeneza akarudi katika hali yake ya awali na kuanza kuaminiwa na familia na marafiki sio masihara... tumeona ubunifu wa kazi nzuri wanazozifanya, huku akizionyesha mfano wa kazi hizo," alisema Dk. Saada.

Naye Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Khadija Khamis Rajab, alisifu jitihada zilizoonyeshwa na mkurugenzi huyo na kumwomba kuendelea kutoa ushirikiano na ushauri pale panapohitajika.

Kwa upande wake, Kheriyangu alisema ushirikiano alioupata umemwezesha kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Kheriyangu alisisitiza kuwa maamuzi yote aliyokuwa akiyatoa yalikuwa yanapitia kwenye vikao kazi kwa pamoja, jambo ambalo limeiwezesha tume kupata mafanikio makubwa katika utendaji wa majukumu yake.

Mkurugenzi Mtendaji mpya wa tume hiyo, Luteni Kanal Burhani Nassoro, aliahidi kushirikiana na watendaji na wafanyakazi ikiwa ni pamoja na kuendeleza mazuri yote yaliyoachwa na mtangulizi wake kubuni mbinu mpya katika kusimamia majukumu ya tume hiyo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**LODGE MPYA YA KISASA NA BAR VINAUZWA MSONGOLA**

Ina Vyumba 9 vyote Self Contained na Ukumbi.
Ukubwa wa eneo SQM 2000.
Bei TShs. 280/= Milioni.
SIMU: 0628 336736.

*Uza,*
*Chenye Thamani Kubwa*
*Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa*
*Tupigie 0782253676*

## TANGAZO LA KUPOTELEWA NA HATI YA KIWANJA

**Mussa Rashid Omary** Anatangaza kupotelewa na Hati Miliki ya kiwanja namba **395 Kitalu** HH Ndala Manispaa ya Shinyanga.
Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Mussa Rashid Omary kwa simu namba **0754577835.**
**Rbnamba/ ShyRb/ 2021, Control Namba 9910823355711.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika mahakama ya mwanzo**
**………..MJINI TANGA**
**Usimamizi wa Mirathi………60……2021**
**Ombi la…………AMINA HAMISI MBWANA ……..Kuteuliwa**

Msimamizi wa mirathi ya marehemu …..KADIRI MOHAMED YUSUF….
Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA
Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 31/5/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 30/6/2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya DODOMA.**

**Kituo cha DODOMA MJINI Mkoa DODOMA.**
**Usimamizi wa mirathi Na…. 2020.**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU SHIKWINUYE EMMANUEL NDOSI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ANNA EVERY SWAI**

**TANGAZO**

(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)
Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 27 mwezi 05 mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 04 mwezi 05 mwaka 2021.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **KAUSHAL KANTI SACHANIA** anatangaza kupotelewa kadi yake ya gari aina yake (IST) yenye usajili Namba **T 249 DPT** yenye **CHASSIS NO NCP650010330.** Kwa yoyote atakaye ona atoe taarifa kituo chochote cha polisi:
**RB Na.MOR/MOR/R-B/228458/2021.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ADAM THOMAS MWANGABA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA VYETI VYA KADI YA TRELLA YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.689 BET** YENYE MAJINA YA KAMPUNI YA ROVTE TECHNOLOGY LIMITED.YEYOTE ATAKAYEVIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.
TAARIFDA YA POLISI
**MBE/MBE/RB/230164/2021**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi NO.127/2021**

**Ombi la MUSTAFA OMARY TAMBA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu KHADIJA MOHAMEDI MGOTO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 25/05/2021 kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe03/05/2021

Sahihi ya Hakimu
Mahakama ya Mwanzo Mjini

## TANGAZO LA KUPOTEA HATI YA NYUMBA

**Nossy Nyakerega** mkazi wa Shirati Rory mkoani Mara, ambaye ni msimamizi wa mirathi ya Nyakerega Jackson Mgono. Anatangaza kupotelewa na hati ya nyumba, kiwanja namba **904 Kitalu HH (HD)** iliyopo Ndala Manispaa ya **Shinyanga.** Kwa yeyeto atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Nossy Nyakerega kwa simu namba **0788089304.**
**RB namba/ SRT/RB/466/2020.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**SHABANI SELEMANI MWANAFUNYO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI ZAKE ZENYE NAMBA ZA USAJILI **T332 BNV FUSO-DAMPER T209 AMP JIEFANG- TRUCK T278 AXR MITSUBISHI** TAARIFA HII IMETOLEWA KITUO CHA POLISI NA KUPEWA KUMB NAMBA- **TAN/TAN/RB/67577/2021, TAN/TAN/RB/67592, TAN/TAN.RB/67583/2021.**

## KUPOTEA KWA HATI YA NYUMBA

**NDUGU YAKUB ISMAIL YAKUB** anatangaza kupotelewa na hati ya Nyumba yenye **TITLE DEED PLOT NO 10 BLOCK 6** huko Kata ya **MADUKANI HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu kwa kumbukumbu namba **DOM/RB/29132/2021**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi**
**NO.130/2021**

Ombi la AHMAD M. MNYANGA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu PILI SALUM MASAWILA
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 06/05/2021 kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe04/05/2021**

*Uza,*
*Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa*
*Tupigie 0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# 30 wauawa kwa shambulio Burkina Faso

**Fada Ngourma,** BURKINA FASO

RAIA wasiopungua 30 wameuawa katika shambulio dhidi ya kitongoji cha kilimo cha Kodyel, eneo la Foutouri, kilomita 145 kutoka mji wa Fada Ngourma katika mkoa wa Mashariki.

Watu wasiojulikana wenye silaha walivamia kijiji hicho, mapema asubuhi ya juzi na kushambulia raia, licha ya watu waliojitolea kwa ulinzi wa taifa, kundi linalosaidia vikosi vya jeshi, kuingilia kati.

Watu hao waliuawa huku nyumba kadhaa zilichomwa moto.

Kwa mujibu wa mashuhuda na vyanzo vya usalama katika eneo hilo, waliotekeleza shambulio hilo walikuwa karibu 300 na shambulio hilo lilidumu saa mbili.

"Walizingira kijiji na kuuwa karibu wanaume wote," anaelezea shahidi aliyetajwa na chanzo chetu.

Wanawake na watoto ndio waliowekwa kando na idadi kamili ya walioathiriwa bado haijajulikana.

Gavana wa mkoa wa Mashariki, alisema kwamba raia wengi waliuawa.

Vyanzo vya usalama vilisema watu wasiopungua 30, pamoja na watu wawili kutoka kundi linalosaidia jeshi waliuawa katika shambulio hilo.

Miongoni mwa raia waliouawa ni mkuu wa kijiji na watu kadhaa wa familia yake.

Kuna watu karibu ishirini waliojeruhiwa pia. Kwa kuongezea, washambuliaji kadhaa walipigwa risasi na kuuawa na kundi linalosaidia jeshi kulinda taifa.

**RFI**



Treni iliyopata ajali jana, baada ya daraja kukatika na kusababisha vifo vya watu 23 na majeruhi 50, wakati treni la chini ya ardhi likipita mjini Mexico. PICHA: AP

# Bill Gates amtaliki mkewe Melinda

**Washington,** MAREKANI

BILIONEA Bill Gates ametangaza kuachana na mkewe, Melinda Gates kwa talaka.

Wawili hao wametalikiana baada ya miaka 27 ya ndoa, wakisema "hatuamini tena tunaweza kuwa pamoja kama wanandoa.

"Baada ya kufikiria sana na kufanya kazi nyingi juu ya uhusiano wetu, tumefanya uamuzi wa kumaliza ndoa yetu," wawili hao walisema hayo kwenye ujumbe waliouandika twitter .

Walikutana kwa mara ya kwanza miaka ya 1980 wakati Melinda alipojiunga na kampuni ya Bill ya Microsoft.

Wanandoa hao, mabilionea wana watoto watatu na kwa pamoja wanaendesha Wakfu wa Bill & Melinda Gates.

Shirika hilo limetumia mabilioni kufadhili kampeni mbalimbali ikiwamo magonjwa ya kuambukizana na kuhamasisha chanjo kwa watoto.

Wawili hao, pamoja na mwekezaji Warren Buffett, wanahusika na mpango wa Ahadi ya Kutoa, ambao unawataka mabilionea kujitolea kutoa utajiri wao mwingi kwa malengo ya kuwafaidi watu

Shirika hilo limetumia mabilioni kufadhili kampeni mbalimbali ikiwamo magonjwa ya kuambukiza na kuhamasisha chanjo kwa watoto.

Wawili haopamoja na mwekezaji Warren Buffett - wanahusika na mpango wa Ahadi ya Kutoa, ambao unawataka mabilionea kujitolea kutoa utajiri wao mwingi kwa malengo ya kuwafaidi watu

Wawili hao walichapisha taarifa hiyo wakitangaza talaka yao kwenye Twitter.

"Katika kipindi cha miaka 27 iliyopita, tumewalea watoto watatu wa ajabu na kujenga wakfu ambao unafanya kazi ulimwenguni kote kuwezesha watu wote kuishi maisha yenye afya, yenye tija," ujumbe huo ulisema

Ni kati ya watu 10 matajiri duniani wanaomiliki mali ya nusu ya watu maskini duniani.

"Tunaendelea kuwa na imani ya pamoja katika lengo hilo na tutaendelea kufanya kazi pamoja kwenye wakfu wetu, lakini hatuamini tena tunaweza kukua pamoja kama wanandoa katika sehemu inayofuata ya maisha yetu.

"Tunaomba nafasi na faragha kwa familia yetu tunapoanza maisha haya mapya."

**BBC**

## Mazungumzo yanaendelea kupata mrithi ufalme wa Zulu

**KwaZulu-Natal,** AFRIKA KUSINI

TANGU kifo cha Mfalme Goodwill Zwelithini, Machi mwaka huu, mmoja wa wajane wake alikuwa ameshikilia nafasi hiyo hadi uteuzi wa mfalme mpya.

Mjane aliyemrithi alifariki wiki iliyopita, akiwa na umri wa miaka 65 na atazikwa kesho, kulingana na mila za kifalme.

Kifo cahke kimedhoofisha umoja ndani ya ukoo wa kifalme na kuibua mvutano katika familiaya kifalme.

Mazungumzo yanaendelea kuongezeka katika kasri ya kifalme ya Nongoma katika mkoa wa KwaZulu-Natal, wakati mazishi ya Malkia Shiyiwe Mantfombi Dlamini Zulu, aliyefariki mwishoni mwa mwezi Aprili, yakikaribia.

Wakati familia ya kifalme hadi sasa ilikuwa imeonyesha picha ya umoja na kushauriana kwa faragha, ili kujua nani atakayechukuwa nafasi ya mfalme, malumbano yameanza kujitokeza hadharani, huku baadhi ya watu wa familia ya kifalme wakifanya mikutano na waandishi wa habari na wengine wakitoa taarifa mbalimbali zinazokinzana.

Baadhi ya watu kutoka familia ya kifalme wameamua kuwasilisha malalamiko yao mahakamani.

Mke wa kwanza kati ya wake sita wa Mfalme Zwelithini, anaomba mahakama kumtambua kama mke mkuu, kwa kuwa ndiye pekee aliyeolewa na mfalme kwa ndoa rasmi inayofuata sheria za nchi.

Katika malalamiko mengine, binti zake wawili wanabaini kuwa wosia ulioachwa na baba yao ulighushiwa na wanaomba usimamishwe.

Goodwill Zwelithini, mfalme wa Zulu tangu mwaka 1971 na ambaye alifariki mwezi Machi akiwa na umri wa miaka 72, alikuwa mfalme mwenye ushawishi mkubwa nchini Afrika Kusini, mamlaka ya maadili kwa Waafrika Kusini milioni 12.

Waziri wa Mambo ya Jadi, ambaye alikuja kutoa heshima zake kwa hayati Malkia, anatumai kuwa amani na utulivu vitarejea haraka ndani ya familia ya kifalme.

**RFI**

## Watu 23 wafa kwa ajali ya treni Mexico

**Washington,** MAREKANI

ZAIDI ya watu 20 wamekufa na wengine kadhaa wamejeruhiwa, baada ya daraja ambako inapita treni kuanguka wakati treni ya chini ya ardhi ikipita katika mji mkuu wa Mexico.

Meya wa Jiji la Mexico City, Claudia Sheinbaum aliwaambia waandishi habari kwamba watu 15 walikufa katika ajali hiyo iliyotokea juzi usiku.

Idara ya ulinzi wa raia wa mji huo, imeandika katika ukurasa wake wa Twitter kwamba, watu wengine wapatao 70 walijeruhiwa.

Idara ya huduma za dharura walikuwa kwenye eneo la tukio kuwaokoa waathiriwa, kutoka kwenye mabehewa katika kituo cha treni cha Olivos.

Ajali hiyo ilitokea wakati treni hiyo ikisafiri kati ya vituo vya Olivos na Tenzonco, Kusini mwa mji huo.

Picha za kamera za mtaani zilioneysha daraja hilo likianguka kwenye barabara iliyokuwa na magari mengi.

**DW**

## HABARI MICHEZO

# LUKAKU:

## SASA NI ZAMU YA UBELGIJI KUTWAA UBINGWA



**MILAN, Italia**

ROMELU Lukaku ana matumaini atakuwa wa moto sana kuisaidia Ubelgiji kwenye michuano ya Euro 2020 baada ya kushinda taji la Ligi Kuu Italia, Serie A, akiwa na Inter Milian.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, amefunga mabao 21 kwenye Serie na kutoa pasi za mwisho 10 msimu huu kwa Inter, ambao walitawazwa kuwa mabingwa wa ligi hiyo Jumapili kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 11.

Ni taji lake la pili kwa mchezaji huyo kwa kipindi chake cha miaka 12 ya soka, baada ya mara ya kwanza kushinda taji la Ligi Kuu ya Ubelgiji akiwa na klabu ya Anderlecht msimu wa 2009-10.

Lukaku, ambaye alijiunga na Inter akitokea Manchester United Agosti mwaka 2019, sasa anapanga kuisaidia Ubelgiji kwenye michuano ya Euro 2020 ambayo itafanyika kuanzia Juni mwaka huu.

"Kushinda mataji na klabu kunakusaini kupata uzoefu wa kutosha kwenye mechi za kimataifa," alisema akiiambia La Tribune.

"Akili yangu ni kuhakikisha tunabeba taji na Ubelgiji, na hivyo ndivyo nilivyojiandaa kwa sasa.

"Hicho ni kitu nilichokikosa kwa kipindi kirefu kwenye maisha yangu ya soka. Nilishakata tamaa mara nyingi.

"Halafu nikajiambia mwenyewe, nimechoka, nina miaka 27, ni wakati wa kubadilika sasa. Lazima tufanye jambo la kupa mataji Ubelgiji."

## KOCHA KUAMUA HATIMA YA BALE

**LONDON, England**

MAJALIWA ya Gareth Bale kuendelea kucheza Tottenham Hotspur yataamuliwa na kocha mpya mwishoni mwa msimu huu, kwa mujibu wa Daily Mail.

Bale anacheza kwa mkopo pale Spurs akitokea Real Madrid ambapo mwishoni mwa msimu huu anatakiwa kurudi kule Santiago Barnebeu kumalizia mwaka wake mmoja uliobaki kwenye mkataba wake.

Kwa mujibu wa ripoti, Mwenyekiti wa Spurs, Daniel Levy, anasubiria kocha mpya atakayetua hapo kuchukua mikoba ya Jose Mourinho aliyetimuliwa ili kuamua hatima ya nyota huyo wa kimataifa wa Wales.

Ripoti zaidi zinasema kwamba, Bale anaweza kuendelea kucheza hapo Spurs kwa mkopo mwingine wa msimu mmoja, badala ya kurudi Madrid.

Bale alikosa nafasi kwenye kikosi cha Madrid chini ya kocha Zinedine Zidane na kuna uwezekano mkubwa wa kubakia hapo Spurs.

Hata hivyo, Spurs inaweza kuwagharimu kiasi cha pauni milioni 12 kumsajili moja kwa moja nyota wake huyo wa zamani.

## HENRY: KUINUNUA ARSENAL SI RAHISI

**LONDON, England**

GWIJI wa Arsenal, Thierry Henry amesema mpango wa bilionea na mwanzilishi wa Kampuni ya Spotify, Daniel Ek kutaka kuinunua klabu hiyo "utakuwa mrefu na si rahisi."



Bilionea huyo mwenye umri wa miaka 38 raia wa Uswisi, alionyesha nia ya kutaka kuinunua Arsenal ambayo amekuwa akiishabikia tangu akiwa na umri wa miaka minane.

Mpango wa Ek kutaka kuinunua Arsenal ulikuja baada ya mashabiki kuandamana kwa mmiliki wake wa sasa kutokana na kujiingiza kwenye Ligi mpya ya Ulaya ambayo baadaye ilifutwa.

Akizungumza na Sky Sports Jumatatu, Henry alisema Ek aliwasiliana na Stan Kroenke na anatarajiwa kutoa ofa ya pauni bilioni 1.8 ili kuinunua klabu hiyo.

Ek anaungwa mkono na magwiji wa Arsenal, Henry, Patrick Vieira na Dennis Bergkamp, lakini bado inaonekana kuwa ni ngumu kama Kroenke atasikiliza ofa hiyo.

"Nafikiri utakuwa mpango wa muda mrefu na si rahisi," alisema Henry.

"Moja ya kitu ninachokitaka ni kuona kwamba Ek anaweza kufanikisha jambo hili, lakini halitakuwa rahisi."

HABARI MICHEZO

## WENGER AUNGA MKONO TAJIRI MPYA ARSENAL

**LONDON, England**



KOCHA wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger, amedokeza kuwa yuko tayari kuungana na bilionea mwanzilishi wa Spotify, Daniel Ek pamoja na wachezaji wake watatu wa zamani, katika zabuni ya Pauni bilioni 1.8 kuinunua klabu hiyo kutoka kwa Stan Kroenke.

Kwa mujibu wa mtandao wa Daily Star, Ek mwenye utajiri unaokadiriwa kuwa Pauni bilioni 3.5 ana mpango madhubuti wa kuinunua Arsenal kwa kushirikiana kwa pamoja na magwiji wa klabu hiyo, Thierry Henry, Patrick Vieira na Dennis Bergkamp.

Wakati mazungumzo juu ya uwezekano wa kuichukua klabu hiyo yakiendelea, Wenger amesema yuko tayari kusaidia timu yake ya zamani "kwa njia yoyote".

Hata hivyo, ripoti imeeleza kuwa wamiliki wa sasa wametoa taarifa wakisisitiza hawana mpango wa kuiuza klabu hiyo hivi karibuni.

## RODGERS AIKATAA RASMI TOTTENHAM

**LONDON, England**

KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers, amesema hana mpango wa kuhamia klabu ya Tottenham Hotspur kuchukua nafasi iliyoachwa wazi baada ya kutimuliwa kwa kocha, Jose Mourinho.

Kwa mujibu wa mtandao wa SkySport, Rodgers anafikiriwa kuwa kwenye orodha ya wanaowania nafasi iliyoachwa na Mourinho, ambaye alipoteza kibarua Jumatatu iliyopita, zikiwa zimesalia siku sita kabla ya fainali ya Kombe la Carabao dhidi ya Manchester City.

Mwingine aliyehusishwa na ukocha Spurs ni Kocha wa RB Leipzig, Julian Nagelsmann, lakini tayari ameshathibitishwa kuwa kocha mpya wa Bayern Munich kuanzia Julai Mosi, mwaka huu.

Aidha, ripoti imeeleza Rodgers hana mpango wa kwenda Tottenham, na kuwa anayafurahia maisha kwenye klabu yake ya sasa, Leicester.

Katika msimamo wa Ligi Kuu ya England, Leicester ipo nafasi ya tatu ikiwa na jumla ya alama 62 ikiizidi pointi tisa Tottenham katika nafasi ya saba yenye jumla ya alama 53.




# SOLSKJAER

## AGOMA UNITED KUMUUZA VAN DE BEEK

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amezikata maini timu zinazomnyatia kiungo wake, Donny van de Beek kwa kusema kuwa mchezaji huyo hauzwi.

Solskjaer ana imani raia huyo wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 24, atakuwa mchezaji muhimu United licha ya kutopata nafasi ya kutosha uwanjani.

De Beek amecheza dakika 330 tu katika Ligi Kuu England msimu huu na amekuwa hana nafasi ya kutosha kwenye kikosi hicho.

Nyota huyo alishabainisha mpango wake wa kutaka kuondoka ndani ya klabu hiyo, ili aweze kupata sehemu ya kucheza mara kwa mara.

De Beek alinukuliwa akisema kwamba, anataka kuiomba klabu hiyo kumruhusu kuondoka mwishoni mwa msimu huu ili kwenda kutafuta sehemu nyingine ambayo atakuwa na muda mwingi zaidi wa kucheza.

Klabu ya As Roma ya nchini Italia imekuwa ikimtaka mchezaji huyo kwa udi na uvumba, lakini akili yake inamtuma kutaka kurejea katika timu yake ya zamani ya Ajax alipotokea kabla ya kuja United msimu huu.

"Naamini de Beek atakuwa mchezaji muhimu kwa Manchester United, sidhani kama anaweza kuamua kuondoka hapa," alisema Solskjaer akinukuliwa na Sky Sport.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# POCHETTINO AKATA TAMAA PSG KUMBAKISHA MBAPPE

Liverpool, Manchester City na Real Madrid zatajwa kukaa mguu sawa kuanza mbio za saini yake, huku...

**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Paris Saint-Germain, Mauricio Pochettino, amekiri kwamba, hana uhakika kama Kylian Mbappe atabaki kwenye timu hiyo wakishindwa kubeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

Mkataba wa Mbappe utafika tamati 2022 na alipoulizwa kuhusu hatima ya mshambuliaji huyo, Pochettino alitoa maelezo kwamba PSG, watafanya kila kitu kuhakikisha anabaki.

"Hilo ni swali linalomhusu Kylian na si mimi. Tumepoteza mechi lakini bado kuna mechi ya marudiano na mambo ya ajabu yamekuwa yakitokea kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya," alisema Pochettino kabla ya mchezo wa jana Jumanne dhidi ya Man City.

"Nilishasema huko nyuma, lakini klabu na mimi tunafanya kwa kila tunaloweza kuhakikisha anabaki kwa miaka mingi.

"Klabu inafanyika kazi jambo hilo na Kylian Mbappe anafuraha kuwa nasi. Tuna mwezi mmoja umebaki kwenye michuano ili kufikia matarajio yetu na bado tupo kwenye mbio."

Liverpool ni klabu ya kwanza ambayo imekuwa ikihusishwa kunasa huduma ya Mbappe na kocha Jurgen Klopp ni shabiki mkubwa wa mchezaji huyo.

Mbappe naye amekuwa akiizungumzia vizuri Liverpool chini ya Klopp, akisema: "Kile wanachokifanya Liverpool ni balaa. Wamekuwa kama mashine."

Real Madrid ni timu nyingine ambayo imekuwa ikihusishwa sana na Mbappe na kwa mujibu wa gazeti la Hispania la Sport, tatizo la kiuchumi linalowakabili 'Los Blancos' hao haliwezi kuwazuia kumsajili.

Kwa mujibu wa ripoti, Real Madrid wapo tayari kumtoa beki Raphael Varane na mshambuliaji Vinicius Junior kwenda PSG kama ofa ya kumchukua Mbappe ili kushusha bei anayouzwa.

Mbappe mwenyewe huko nyuma aliwahi kusema kocha wa sasa wa Real Madrid, Zinedine Zidane ndiye aliyekuwa shujaa wake wa kwanza na anaona kuna uwezekano wa kwenda kufanya naye kazi Bernabeu.

Pia Man City inayonolewa na Pep Guardiola ambayo itakwenda kuachana na straika wake, Sergio Aguero mwishoni mwa msimu huu mkataba wake utakapokwisha, wanamtaka Mbappe.

Kwa mujibu wa gazeti la Ufaransa, Le Parisien, Man City ni miongoni mwa klabu zinazovutiwa na mpango wa kumsajili Mbappe, hivyo wapo tayari kuvunja benki kukamilisha jambo hilo.

## KWA UFUPI

**DORTMUND KUMUACHIA SANCHO**

KLABU ya Borussia Dortmund itamuachia mchezaji wa kimataifa wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 21, kuondoka klabuni hapo kwa kitita cha pauni milioni 87. **(Mail)**

**LEWANDOWSKI ANUKIA KUUZWA**

WAKALA wa Robert Lewandowski, Pini Zahavi anajiandaa kutia msukumo kwa Bayern Munich kumpa mkataba mpya mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Poland au kumuuza katika klabu ambayo itaweza kummudu. (Bild)

**TONEY AWANIWA EPL**

LEICESTER City na Everton ni miongoni mwa klabu zinazojiandaa na mchakato wa kumnasa mshambuliaji wa Brentford, Ivan Toney mwenye umri wa miaka 25. **(Athletic)**

**BALE KUBAKISHWA SPURS**

MWENYEKITI wa klabu ya Tottenham, Daniel Levy, atampa kocha ajaye wa klabu hiyo nafasi ya kumsainisha tena mshambuliaji wa Wales, Gareth Bale mwenye umri wa miaka 31, kwa mkopo kutoka Real Madrid kwa msimu wa 2021-22. **(Mail)**

**WATZKE AMFUNGUKIA HAALAND**

MTENDAJI Mkuu wa klabu ya Borussia Dortmund, Hans-Joachim Watzke, amerejelea msimamo wa klabu hiyo kwamba mshambuliaji wa Norway, Erling Braut Haaland, ambaye amekuwa akihusishwa na Manchester United, Liverpool, Manchester City, Chelsea, Barcelona na Real Madrid- hatauzwa. **(Metro)**

**DOEKHI AWINDWA NEWCASTLE**

NEWCASTLE United na Atlanta zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili mlinzi wa Vitesse Arnhem, Danilho Doekhi mwenye umri wa miaka 22, ambaye anahusishwa na taarifa za kutupiwa jicho na Norwich City. **(De Telegraaf)**

**YOUNG AWANIWA WATFORD**

KLABU ya Watford imefanya mawasiliano na Inter Milan juu ya mlinzi wa England, Ashley Young mwenye umri wa miaka 35, kuhusu kurejea kwenye klabu hiyo, ambako alianzia kucheza. **(Watford Observer)**

**GLAZER KUIUZA MAN UNITED**

FAMILIA ya Glazer inaweza kushawishiwa kuiuza Manchester United, na wataiuza kwa kiasi cha pauni bilioni 4. **(Times)**

**NICE WAMTAKA LINGARD**

KLABU ya Nice ya Ufaransa, imeendelea kuonyesha nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Manchester United, Jesse Lingard baada ya kumkosa alipojiunga kwa mkopo West Ham. **(Sky Sports Italia)**

**SCHAR KUFUNGWA NEWCASTLE**

NEWCASTLE United ina nia ya kumuongezea mkataba mchezaji wa kimataifa wa Uswisi, Fabian Schar mwenye umri wa miaka 29. **(Northern Echo)**

**SPURS WAMTAKA AARONS**

KLABU ya Tottenham Hotspur imejaribu kufanya mawasiliano kwa ajili ya mchezaji wa Norwich na mlinzi wa England anayechezea kikosi cha umri wa chini ya miaka 21, Max Aarons, 21. **(Football Insider)**

HABARI MICHEZO

# ODHIAMBO APEWA MIKOBA YA BARAZA BIASHARA UNITED

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa timu ya Biashara United umeingia makubaliano na Kocha Mkenya Patrick Odhiambo, kukinoa kikosi hicho kwa michezo iliyobaki ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Odhiambo sasa anachukua nafasi ya aliyekuwa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Francis Baraza, ambaye ametimkia Kagera Sugar hivi karibuni.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Biashara United, Selemani Mataso, alisema wamemtambulisha Odhiambo kuongoza kikosi cha timu hiyo kwa makubaliano maalum.

Alisema makubaliano ambayo wameingia ni kumalizia mechi zilizobaki za ligi hiyo na baada ya kumalizika kwa msimu huu watampa mkataba wa kuendelea na kazi aliyoanza.

"Tumeingia makubaliano na Odhiambo ya kumalizia michezo ya msimu huu, baadaye atasaini mkataba rasmi kuendelea na majukumu ya kuongoza kikosi cha timu yetu kwa muda ambao tutakubaliana.

"Hatua hii ni baada ya kanuni za Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kutoruhusu kocha wetu msaidizi Marwa Chamberi kuendelea kuongoza kikosi chetu kwa mechi zilizobaki," alisema Mataso.

Alisema Odhiambo alianza kazi rasmi jana, kukinoa kikosi cha timu hiyo kumalizia msimu huu wa ligi, akichukuwa nafasi ya Baraza. Odhiambo mwenye leseni B ya CAF, anajiunga na Biashara United kuwa kocha mkuu baada ya kuachana na Klabu ya Kakamega Homeboyz ya Kenya.

MILIKI...




Mchezaji wa timu ya U11 Bulls Academy DarYC, Kapakwashe Zengeni, akimiliki mpira katikati ya mabeki wa timu ya Mikocheni United kwenye mchezo wa kirafiki uliozikutanisha timu hizo viwanja vya Masaki Sports Park jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Straika Gwambina mawindoni Yanga

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA hatari wa Gwambina FC, Meshack Abraham, amesema kuna klabu zimekuwa zikimfuata na kumshawishi kujiunga na timu zao, lakini ameziambia zisubiri hadi Ligi Kuu Tanzania Bara itakapomalizika ndipo ataamua.

Mchezaji huyo ambaye mpaka sasa ameshapachika mabao tisa, akizidiwa matatu tu na kinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Prince Dube wa Azam FC mwenye mabao 12, amesema tayari ofa kadhaa zipo mikononi mwake, lakini ameweka wazi wakati huu si wa kuzungumzia hayo kwa sababu anaipambania timu yake ya Gwambina kukaa sehemu salama kwenye msimamo wa ligi.

**"Ni kweli kabisa, kuna timu ambazo zimesha wasilisha ofa na zinataka kunisajili. Kwa sasa siwe zi kuzitaja, nimeshasema kuwa wote wanaohitaji huduma yangu wasubiri ligi imalizike kwa sababu nataka kwanza niipe mafanikio timu yangu," alisema mchezaji huyo.**

Wakati straika huyo akikataa kuzitaja, habari zinaeleza kuwa klabu ya Yanga na KMC zimeshajitosa kuwania saini ya mchezaji huyo ambaye ni mmoja wa wachezaji wachache wa Kitanzania wenye uwezo wa kufunga mabao.

Yanga ambao inahitaji kujiimarisha msimu ujao, moja kati maeneo ambayo yana matatizo msimu huu ni kwenye nafasi yake ya ushambuliaji na mchezaji huyo anadaiwa kuwa ndiye chaguo la kwanza kwa sababu ni mzawa na pia tayari ameshaifahamu Ligi ya Tanzania.

Hata hivyo, huenda klabu zingine pia zikajitosa kadri atakapokuwa anaendelea kufunga au wakati wa usajili utakapoanza.

Mabao yake ndiyo yaliyoifanya Gwambina mpaka sasa kuwa kwenye nafasi ya 12, ikiwa na pointi 30.

# Serikali kuingilia kati pambano la Dulla Mbabe, Kiduku

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeahidi kutoa ushirikiano katika kufanikisha pambano la masumbwi kati ya mabondia mahiri nchini, Twaha Kiduku na Dulla Mbabe litakalofanyika Julai 24, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Hayo yalisemwa juzi na Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbas, wakati wa futari kwa mabondia iliyoandaliwa na Wakala wa Michezo wa PeakTime, Lugalo jijini Dar es Salaam.

**"Hili tunalibeba, hakuna kusubiri na natoa wito kwa wadhamini kujitokeza kutumia nafasi hii kujitangaza kwa kuleta maslahi kwa washiriki," alisema Dk. Abbas.**

Aliongeza kuwa mbali na kutoa ushirikiano, pia aliahidi kufikisha ombi kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuwa mgeni rasmi katika pambano hilo.

Aidha, alisema wameanza kutenga fedha kidogo kidogo ili kusaidi wanamichezo wanaosafiri nje ya nchi kuwakilisha Taifa.

Naye Mwakilishi wa PeakTime walioandaa futari hiyo, Kapteni Selemani Semunyu, alisema maandalizi kuelekea pambano hilo yako sawa na uwapo wa waziri mkuu utaupa hadhi mchezo huo na kufungua fursa nyingi kwa wachezaji ambao wengi hutoka familia duni.

"Tunaendelea kutafuta wadhamini ili ikifanikiwa waziri mkuu aje kukabidhi gari, zawadi ambayo tunaamini itakuwa chachu katika mchezo huo na tunaamini wadhamini watajitokeza," alisema Kapten Semunyu.

Kwa upande wa Mwakilishi wa Kamisheni ya Kusimamia Ngumi za Kulipwa Tanzania (TPBRC), Yahaya Poli, ameipongeza PeakTime na kuwaomba wadau wengine kuiga mfano huo kwani unaipa heshima tasnia hiyo ya ngumi.

Michezo

Jumatano Mei 5, 2021

Nipashe



POCHETTINO AKATA TAMAA PSG KUMBAKISHA MBAPPE HABARI UK 22

## JUMAMOSI TENA...




Raha utamu ya mtifuano wa beki wa kushoto wa Simba, Mohamed Hussein 'Tshabalala' na winga wa kulia wa Yanga, Tuisila Kisinda, ambayo inatarajiwa kushuhudiwa tena kwenye mechi ya 'dabi' Jumamosi wakati timu hizo zitakapokutana Jumamosi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kwenye mechi ya Ligi Kuu mzunguko wa pili. Mzunguko wa kwanza timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: MAKTABA**

# Simba, Yanga kwani wenyewe wanasemaje

●●●Msikie Mwameja, Mmachinga wafungukia 'dabi', TFF yataja waamuzi, makocha nao...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

HUKU homa ya 'dabi' ya watani wa jadi ikizidi kupanda na makocha wa pande zote kila mmoja akieleza wapo tayari kwa mechi hiyo itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumamosi, wachezaji nyota wa zamani wa timu hizo wametoa tathimini yao kuelekea mtifuano huo wa kibabe.

Kipa wa zamani wa Simba, Coastal Union na timu ya Taifa, Taifa Stars, Mohamed Mwameja, amewataka wachezaji wa Simba na Yanga kuachana na presha za nje ya uwanja, badala yake kucheza soka safi ili kudhihirisha kuwa wao ni wachezaji wa timu kubwa na hawajakosea kuwa hapo.

Wakati Mwameja akisema hayo, straika wa zamani wa Yanga, Mohamed Hussein 'Mmachinga', amesema mara nyingi mechi za watani wa jadi hazina mwenyewe, lakini zina vimbwanga vingi nje ya uwanja kuliko ndani.

"Mimi nawataka wachezaji wa timu zote mbili wawatendee haki mashabiki watakaokuwa uwanjani na wale ambao watakuwa wanalitazama pambano hilo kwa kucheza soka safi na si la vurugu, lakini waachane na presha zilizo nje ya uwanja. Sana sana ni hawa wachezaji chipukizi ambao hawana uzoefu sana na mechi hizi, timu yoyote itakayojipanga vizuri au wachezaji wake kucheza vizuri siku hiyo, itashinda," alisema Mwameja, Tanzania One wa kuanzia wa miaka ya 1990.

Kuhusu mambo ya nje ya uwanja, Mwameja alisema yapo kwa sababu timu hizo zimejengwa katika misingi hiyo tangu mwanzo, hivyo ni ngumu kuacha moja kwa moja.

"Mimi nina mikasa mingi, unajua kwenye timu hizi kama hukufanya mambo yao hayo wanakuwa na mashaka na wewe. Wanakuona msaliti kuwa unaweza kuuza mechi na si mwenzao, hivyo huwezi kuyakataa. Lakini mara nyingi yanafanyika nje ya uwanja, ndani inabaki ni kazi ya mwalimu. Inabaki ni kutekeleza yale ambayo kocha amewafundisha wachezaji na si vinginevyo tena," alisema.

Kwa upande wa Mmachinga, alisema mechi za Simba na Yanga huwa hazitabiriki na haijalishi timu gani ni bora kuliko nyingine au inapitia mazingira mazuri au mabaya.

Kuhusu dhana ya ushirikina kwenye mechi hizo, straika huyo alisema zipo, lakini hufanyika nje, huku ndani ya uwanja ni mwalimu ndiye hufanya kazi yake.

"Tangia zamani vipo. Siku hizi siyo sana, vyote vina nafasi kwa sababu kuna wachezaji vinawaweka sawa kisaikolojia, bila hivyo hacheza mpira, kwa hiyo akiwa sawa kichwani anamsikiliza vizuri mwalimu wake na kufuata maelekezo," alisema staika huyo wa muda wote kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara akiwa na mabao 26 ambayo hajavukwa na mchezaji yeyote mpaka sasa.

Kwa upande wa makocha, Kocha Mkuu wa Simba, Mfaransa Didier Gomes, alisema ubingwa utaamuliwa na mechi hiyo, wao wamejipanga kushinda ili kujihakikishia nafasi ya kutetea taji lao.

Lakini Kocha Msaidizi wa Yanga, Razak Siwa, yeye alisema: "Hali ya kikosi chetu ipo vizuri, tunaendelea na programu za mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi hiyo ya dabi, tunaamini tufanya vizuri kwa kuwa bado hatujakata tamaa ya ubingwa".

Wakati huo huo, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), limetangaza waamuzi watakaosimamia mchezo kuwa ni Emmanuel Mwandembwa kutoka Arusha ambaye atakuwa mwamuzi wa kati huku wa akiba akiwa ni Ramadhani Kayoko wa Dar es Salaam.

Mwamuzi wa pembeni namba moja ni Frank Komba kutokea Dar es Salaam na namba mbili akiwa ni Hamdani Said wa Mtwara.

Simba watakuwa wenyeji wa mchezo huo huku wakiwa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo na pointi zao 61, nne mbele ya Yanga iliyopo nafasi ya pili lakini yenyewe ikiwa michezo miwili mbele.

## TUHUMA RUSHWA YANGA, PRISONS ZATUA BUNGENI

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SAKATA la rushwa kwenye michezo ya soka limeibuka bungeni jana, baada ya Mbunge wa Kinondoni (CCM), Abbas Tarimba, kuzungumzia tuhuma zilizotolewa nahodha timu ya Tanzania Prisons, Benjamin Asukile, ambaye alidai kuwa timu yake ilitaka kuhongwa Sh. milioni 40 na Yanga.

Akiuliza swali la nyongeza bungeni jana, Tarimba alisema katika mechi kati ya Prisons na Yanga iliyochezwa wiki iliyopita mkoani Katavi ziliibuliwa tuhuma na Prisons kudai timu yake ilitaka kuhongwa fedha hizo ili kuachia mchezo huo.

"Baada ya kumalizika na mabigwa wa kihistoria, Yanga kupata ushindi, kiongozi wa Prisons alinukuliwa na vyombo vya habari timu yake ilikuwa katika kuhongwa Sh. milioni 40 ili kuachia mchezo huo. Je, serikali haioni taarifa kama hizi ndio za kuanzia kuhoji watu kama hawa ili kupata ukweli," alihoji.

Akijibu maswali ya wabunge, Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Innocent Bashungwa, alisema serikali inapambana na vitendo vya rushwa kwenye michezo kwa nguvu zote na inahakikisha inashirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kudhibiti rushwa.

"Serikali haitafumbia macho timu inayotumia rushwa kujipatia ushindi," alisema.

Awali, akijibu swali la Mbunge huyo, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, alisema kumekuwa na kasumba ya viongozi wa timu mbalimbali nchini hasa wanapofungwa na timu ya Yanga kwa halali kutoa kauli kuwa walihongwa.

"Ifike mahali viongozi wa timu hizi na Watanzania wakubali Yanga ni timu bigwa na bora Afrika kwa hiyo wanapofungwa wakubali matokeo," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Mlalo (CCM), Rashid Shangazi, alisema vitendo vya rushwa vimekithiri sana katika mchezo wa soka hapa nchini.

"Je, ni kwa kiasi gani serikali inakabiliana na kudhibiti hali hiyo?"Alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Ndejembi, alisema serikali kupitia TAKUKURU imekuwa ikikabiliana na vitendo vya rushwa kwenye mchezo wa soka kwa kufanya uchambuzi wa mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya viingilio katika mechi za mpira wa miguu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042